


Jumatatu Oktoba 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581465 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# Inatisha

• **Ajali** barabarani zaua watu 133 kila mwezi nchini, majeruhi maelfu; Trafiki walia na bodaboda...*Endelea ukurasa 16*

UKURASA WA 17

**KIINI MIGOGORO YA ARDHI ZANZIBAR**

SHEHA wa Paje Mkoa wa Kusini Unguja, Muhammed Rajab Makame, amesema umaskini wa kipato kwa wananchi...

UKURASA WA 18

**WAFANYABIASHARA WAKUBWA KUPEWA MKOPO HADI BIL.300/-**

BENKI ya NMB imewahakikishia wafanyabiashara wakubwa Kanda ya Dar es Salaam wanaohudumiwa na taasisi...

UKURASA WA 19

**2,220 WAFARIKI MASHAMBULIZI YA ISRAEL PALESTINA**

WIZARA ya Afya ya Gaza imesema mashambulizi ya Israel katika ukanda wa Gaza yameshawaua zaidi ya watu 2,200...



## Samia azindua shule 300 akiwapa ujumbe maalum wazazi

UKURASA 2

## Shule mpya ya Kiboriani toka zama za hali mbaya






Madarasa mapya yaliyojengwa na serikali katika Shule ya Msingi Kiboriani, wilayani Mpwapwa, Dodoma. Kila darasa lina madawati mapya 15. Awali (picha ya chini) wanafunzi waliketi sakafuni, vumbi na baridi vilitawala sakafu. **Picha zaidi Uk. 4. PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

UKURASA WA 3

**'Tolle** wa ITV atakumbukwa kwa uchapakazi'

UKURASA WA 15

**Hatima** madaktari tarajali bado giza, waiangukia serikali



UKURASA WA 16

**Idadi** viongozi CCM waliofariki dunia kwa ajali yaongezeka



Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata

## Ufafanuzi mfanyabiashara anayedai milioni 960/- tuhuma dhidi ya TRA

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI HATAKI KUPOTEZA TENA UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Sagara baada ya kuwasili mkoani Singida kwa ajili ya ziara ya kikazi jana. **PICHA: IKULU**

# Ufafanuzi mfanyabiashara anayedai milioni 960/- tuhuma dhidi ya TRA

KATIKA toleo letu Na. 0581462 la Ijumaa iliyopita, tulikuwa na habari yenye kichwa cha habari kilichosomeka "Kashfa nzito TRA" kikifuatwa na vidokezo "mfanyabiashara adai ina mfumo wa kuchepusha makusanyo, alia kutozwa Mil. 960/-, yenyewe yajibu".

Tumebaini kuna makosa katika maneno "alia kutozwa Mil. 960/-" kwa kuwa mfanyabiashara huyo katika madai yake hajalalamika kutozwa kiwango hicho cha fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), bali anadai kwamba kiasi hicho cha fedha ni hasara ambayo ataipata ikiwa TRA itaendelea na msimamo wake kutokana utata ulioibuka katika mfumo wa Forodha wakati wa uingizaji bidhaa zake toka nje ya nchi.

Kimsingi, habari hiyo imetokana na madai ya mfanyabiashara Emmanuel Gadi anayeituhumu TRA kutengeneza mfumo wa kuingiza mizigo nje ya mfumo wa serikali.

Hata hivyo, uongozi wa TRA mwishoni mwa wiki ulikanusha madai ya mfanyabiashara huyo, ukisisitiza mamlaka hiyo haina mfumo mwingine unaoendesha wa kuingiza mizigo nje ya mfumo wa Forodha wa TANCIS.

"Tunapenda kuufahamisha umma kuwa TRA haina mfumo wowote mwingine zaidi ya mfumo uliopo wa TANCIS ambao unatumika kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACCMA), alisema Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Stephen Kauzeni alipofafanua Alhamisi iliyopita.

Kupitia ujumbe wa video fupi iliyosambaa katika mitandao ya kijamii wiki iliyopita, mfanyabiashara huyo anadai mfumo huo ulianza kutumika mwaka 2018 (miaka mitano iliyopita). Anadai unafanana na ule uliotengenezwa na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mkoani Mbeya.

Mfanyabiashara huyo anadai TRA ilitengeneza mfumo huo kwa makusudi ili ikusanye mapato kwa maslahi ya binafsi ya baadhi ya watu na kuisababishia serikali hasara ya mabilioni ya shilingi ambazo zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi.

"TRA wanaacha kodi ya karibu Sh. milioni 400 kutokana na kuficha makosa yao na wananisababishia mimi hasara ya Sh. milioni 968 kwa ajili ya kuficha makosa yao. Ninaomba nirekebishiwe nyaraka zangu ili nilipe ushuru unaostahili wa Sh. milioni 400 ambao niko tayari kulipa," anasema.

Gadi anadai kuwa tangu mwaka 2018, mfumo huo ambao anautaja uko kinyume cha Sheria za Forodha, umekuwa unalazimisha wafanyabiashara kuingiza nchini mizigo kwa jina la wakala, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria za Forodha.

Anadai kuwa: "Mwaka jana kampuni ya Tosh Logistic Ltd iliingiza mizigo kwa utaratibu huohuo ambao TRA waliutengeneza na baadaye walibaini kwamba utaratibu ule unakwenda kinyume cha Sheria za Forodha.

"TRA wametoa vibali kwa kampuni mbili kuingiza mizigo ya wafanyabiashara kwa majina ya kampuni zao. Kampuni hizo ni Tosh Logistics na Opo Agency, jambo ambalo halikubaliki kwa mujibu wa Sheria za Forodha," anadai.

Mfanyabiashara huyo anadai kuwa mwaka jana aliagiza mizigo kupitia kampuni ya Tosh Logistics na baada ya mzigo kufika kwenye ghala lao Mkuranga, mzigo huo ulipata ajali ya kuungua hivyo kulazimika kupeleka madai kwenye bima ambayo iliomba nyaraka zilizotumika kuingiza mzigo huo ili walipe fidia.

"Uchunguzi wa kina ulifanyika kuhusu ile ajali na baada ya kukamilika, bima ilituomba nyaraka tulizotumia kuingiza mzigo na mimi nikaenda kwa wakala wangu Tosh Logistics, lakini alikataa, akasema hawezi kuzitoa kwa sababu kuna utaratibu mwingine," anadai.

Gadi aanadai wakala - Tosh Logistics aliiandikia kampuni ya bima kuhusu namna mzigo huo ulivyoingia nchini na baada ya Kampuni ya bima kupokea barua kutoka Tosh Logistics haikuridhika na taratibu zilizotumika kuingiza mzigo huo na matatizo yalianzia hapo.

"Ile kampuni yangu ya bima haikuridhika kabisa na utaratibu uliotumiwa na Tosh kuingiza mizigo yangu na ilisema Sheria za Forodha ni Sheria za Afrika Mashariki siyo sheria za Tanzania peke yake kwa hiyo wakasema lazima wafuate utaratibu huo ili kukamilisha malipo yangu na walisema waziwazi kwamba shida ni utaratibu tu ukikamilika watanilipa.

"Baada ya kuona hivyo mimi na kampuni ya bima tuliiandikia barua TRA kuomba ufafanuzi kuhusu utaratibu uliotumika kuingiza mizigo yangu nchini cha kushangaza TRA walipokiona kibali chao wenyewe walitamani kukimbia lakini baada ya siku mbili walianza kufanya uchunguzi," anadai.

Gadi anaeleza kuwa baada ya siku kadhaa TRA ilitangaza kuwakumbusha wananchi kuhusu Sheria za Forodha na aliambiwa atulie kwani kuna utaratibu unafanyika ili apewe fedha zake na Wizara ya Viwanda na Biashara.

"Jambo hili lilinishtua sana, kwamba nipewe fedha zangu na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa msingi upi? Nikaona kweli kuna kitu nikatulia kidogo wakati ule mgogoro wa Kariakoo uliibuka mara tu walipotangaza zile Sheria za Forodha," anasema.

Anadai kwa kawaida TRA huwa wanajibu barua za wafanyabiashara ndani ya wiki moja, lakini barua yake ilikaa zaidi ya miezi mitano bila kupata majibu kwa kile alichoeleza kuwa cha kumjibu kwa kuwa makosa yalikuwa upande wao.

Katika ufafanuzi wake, Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Stephen Kauzeni, alidai Emmanuel Gadi alifikisha malalamiko yake kwa njia ya barua tarehe 27 Februari mwaka huu, akidai kupewa uthibitisho na TRA wa kuingiza mzigo wa vifurushi 471 vya Toner Cartridges kupitia kampuni ya Tosh Logistics Ltd.

Alidai TRA ilifanya uchunguzi wa kutosha na kuthibitisha hapakuwa na mzigo wowote ulioingizwa nchini kwa jina la Wintech Tanzania Ltd wa vifurushi 471 vya Toner Cartridges kupitia kadhia yenye namba TZDL - 22-1382193 ya tarehe 18 Agosti 2022 kama anavyodai.

Alidai TRA ilimjibu mhusika kupitia barua yenye kumbukumbu namba CF 8/92/01 ya tarehe 25 Julai mwaka huu, ikimjulisha kuwa kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa House Bill of Lading na kutoonekana kwa mzigo huo kwenye kadhia iliyowasilishwa na kampuni ya Tosh Logistics Ltd, TRA isingeweza kuthibitisha kuingizwa kwa mzigo huo nchini.

"Kupitia taarifa ya Emmanuel Gadi aliyoitoa kwenye vyombo vya habari, tumebaini kuwapo kwa viashiria vya ukwepaji kodi kwani ni dhahiri kuwa mzigo wake uliingizwa kwa njia za magendo," alidai Meneja Kauzeni.

Alimtaka mlalamikaji kuwasilisha nyaraka na uthibitisho wa kampuni yake kuingiza mzigo huo nchini mara moja ili hatua stahiki zichukuliwe.

*Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza kutokana na maneno "alia kutozwa Mil. 960/-".

**Mhariri**

## Samia azindua shule 300 akiwapa ujumbe wazazi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan amezindua Shule ya Msingi Imbele na Sekondari Mwanamwema mkoani Singida kwa niaba ya shule mpya 302 zilizojengwa nchi nzima kupitia Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi (BOOST) na Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Akizungumza na wananchi wa Manispaa ya Singida baada ya kuzindua shule hizo ambazo serikali imetoa Sh. bilioni 230 wakati wa ziara yake mkoani Singida jana, Rais alisema serikali imedhamiria kuboresha elimu na kumwandaa mtoto kuanzia awali mpaka elimu ya juu.

Alisema kuwa baada ya kujenga shule hizo kupitia miradi hiyo, ni muhimu wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni kupata elimu kwa kuwa miundombinu mizuri ya shule za awali, msingi na sekondari ipo na inatosheleza.

"Wazazi wenzangu, kazi yetu tuhakikishe watoto wanasoma, wanakwenda shuleni kupata elimu. Tumeanza na elimu ya awali, tunataka kuwaandaa watoto kuanzia miaka minne, tuzitunze shule hizi kwa kuwa miradi hii ni yetu," aliagiza.

Akiwa katika Jimbo la Manyoni Mashariki, Rais Samia aliwapongeza wakulima wa mkoa huo kwa kuzalisha mazao kama mahindi, mbaazi na alizeti kwa wingi na kuchangia upatikanaji chakula na kuuondoa mkoa katika mikoa yenye lishe duni.

Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema kwa kipindi cha kuanzia 2005 hadi 2026, serikali imetenga Sh. trilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi wa shule za awali, msingi na sekondari kupitia miradi ya BOOST na SEQUIP.

Alisema hadi sasa zimekwishatolewa Sh. bilioni 230 ambazo zitatumika kujenga shule za msingi 302, shule za awali 364 na madarasa 2,929.

Mchengerwa alisema hadi kufikia Septemba mwaka huu, shule mpya 194 zimejengwa, shule za awali 294 zimejengwa na madarasa 2,303. Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Dk. Elpidius Baganda, alisema katika utekelezaji ujenzi wa miradi ya BOOST, upanuzi wa shule za kidato cha tano kupitia serikali kuu na mradi wa SEQUIP, mkoa ulipewa Sh. bilioni 21.3.

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida alisema mkoa ulipokea kiasi cha Sh. bilioni 9.3 kwa ajili ya ujenzi wa shule moja ya wasichana na shule nane za kata.

Alisema katika awamu ya kwanza ya mradi wa SEQUIP, mkoa ulipokea Sh. bilioni 4.23 kwa ajili ya ujenzi wa shule tisa za kata na kwamba shule za awamu ya kwanza zimeshasajiliwa.

HABARI KITAIFA

# Tolle wa ITV atakumbukwa kwa uchapakazi

**Na Halfani Chusi**

WAANDISHI wa habari nchini wameungana na familia kumlilia aliyekuwa Mwandishi wa Habari wa ITV mkoani Dodoma, Shaban Tolle (pichani), aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Mama Ngoma iliyopo Mwenge mkoani Dar es Salaam.

Tolle alifikwa na umauti wakati akipambania afya yake kutokana na ugonjwa wa saratani uliokuwa ukimsumbua kwa muda mrefu.

Taarifa ilitolewa jana kuhusu kifo chake ilieleza kuwa mwili wake umehifadhiwa katika Hospitali ya Jeshi Lugalo, kwa ajili ya mazishi yanayofanyika leo saa saba mchana makaburi ya Kisutu Upanga, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Matukio wa ITV, Steven Chuwa, alisema taratibu za mazishi zinaendelea nyumbani kwa kaka yake, Idd Nassoro, karibu na Msikiti wa Al Maarifa, Mbezi Makonde.

Kuhusu taratibu za mazishi alisema mwili utachukuliwa katika Hospitali ya Lugalo na kwenda nyumbani kwa kaka yake kwa ajili ya ibada kabla ya kupumzishwa katika nyumba ya milele.

Katika makundi songezi na kwenye mitandao ya kijamii, wanahabari walimlilia mwanatasnia mwenzao huku kila mmoja akimwelezea namna alivyokuwa mahiri kwenye kazi.

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa ambaye kitaaluma ni mwandishi wa habari aliandika katika ukurasa wake wa Facebook "Poleni wana familia wote wa ITV na wote walioguswa na kifo cha Shaban Tolle. Mtu pole, mwema, mkarimu na mchapakazi na rafiki wa kila mtu."

"Poleni zenu wote wana tasnia ya habari, binafsi nimesikitishwa sana na msiba wa mpigapicha mwenzangu miaka ya nyuma," aliandika Kibwana Dachi katika kundi la Tasnia ya Habari Tanzania.

Katika ukurasa wake wa Facebook, Mwanahabari Albert Kawogo, aliandika "Tarehe 11, 2004 ulinipokea chumba cha habari ITV wewe na marehemu Julius Nyaisanga, Aboubakary Mlawa na marehemu John Mndolwa (former news coordinator ITV), ndio mlichangia kuja kwangu ITV.

Mwandishi Maggid Mjengwa aliandika "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo chake, amefariki dunia baada ya kupambana muda mrefu na maradhi ya saratani, alitumikia ITV. Nimekutana naye kwenye matukio mbalimbali ya kihabari alikuwa mwelezi, mwenye bidii na nidhamu ya kazi yake."

Richard Mkenda aliandika katika ukurasa wa Mwandishi wa ITV mkoani Morogoro, Idda Mushi, "Kwaheri kamanda wangu uliyenipokea Dodoma, binadamu hatuna jinsi mbele ya mauti, Mungu amekuhitaji kapumzike kwa amani."



Naye Faustine Galafoni aliandika "Nimesikitishwa na kifo cha mwanatasnia mwenzangu na mkongwe katika tasnia tulikaa pamoja tulipiga stori na wakati mwingine alipoelemewa na majukumu aliniagiza kwenda kuchukua matukio na aliniasa sana kujituma."

Mwandishi wa Habari na Mpigapicha wa Chanel Ten, ambaye aliwahi kufanya naye kazi pamoja akiwa ITV Emannuel Chegere, alisema marehemu alikuwa mpole na msikivu.

Marehemu Tolle ameacha mke na watoto wanne.

# Kiswahili chapigiwa chapuo mikutano WB, IMF

**Na Benny Mwaipaja,**
MARRAKECH

TANZANIA imeishauri Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kukifanya Kiswahili kuwa miongoni wa lugha za mawasiliano wakati wa mikutano yake kutokana na kukua kwa lugha hiyo na kutumika kwenye mikutano mingine mingi ya kikanda na kimataifa.

Ushauri huo umetolewa mjini Marrakesh, Morocco na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, wakati wa Mkutano wa 26 wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu kutoka Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika ambazo ni wanachama wa Benki ya Dunia.

Dk. Saada Mkuya Salum, anayeongoza ujumbe wa Tanzania katika mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kwa niaba ya Waziri wa Fedha wa Tanzania, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema ni wakati mwafaka wa kukijumuisha Kiswahili katika mijadala ya taasisi hizo kubwa za fedha duniani kwa kuwa wanachama wake wengi kutoka katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanazungumza lugha hiyo.

"Takribani watu milioni 200 wanazungumza Kiswahili duniani, tumewasilisha ombi hili ikiwa ni jitihada za serikali za kukifanya Kiswahili kuwa bidhaa," alisema Dk. Saada.

Ajenda hiyo itajadiliwa wakati wa Mkutano wa 27 wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika ambazo ni wanachama wa Benki ya Dunia, wakati wa Mikutano ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), itakayofanyika Washington D.C, nchini Marekani, mwezi Aprili, mwakani.

Waliitaka pia benki hiyo kuzihudumia nchi wanachama wake kwa usawa wakati wa majanga ikiwamo matatizo ya mizozo ya kivita kama wanavyofanya kwenye nchi nyingine zenye matatizo kama hayo kwenye mabara mengine, hatua inayokwamisha juhudi za nchi hizo kukabiliana na changamoto hizo na kukwamisha juhudi za kujikwamua kiuchumi.

Mkutano huo umehudhuriwa pia na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu El-maamry Mwamba.







**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

## TANGAZO KWA UMMA

## MIKOPO YA BOTI ZA KISASA ZA UVUVI AWAMU YA PILI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inautangazia umma kuwa imepanga kuwakopesha wavuvi mkopo nafuu (usio na riba) wa Boti za "Fiber" za uvuvi awamu ya pili. Mkopo huu unalenga kuwawezesha wavuvi kufanya uvuvi wa kibiashara.

Boti za urefu wa kuanzia mita 5 , 8, 10, 12 hadi 14 zikiwa na Injini zenye nguvu ya farasi kuanzia 15 hadi 75 kulingana na urefu; uwezo wa kubeba wavuvi 6 hadi 20; uwezo wa kubeba samaki hadi tani 1.5; kifaa cha kufuatilia uwepo wa samaki; kifaa cha kuongoza boti (GPS); vifaa vya kuokolea Maisha na nyavu za uvuvi.

Miongozo ya maombi na vigezo vya kina vinapatikana kwa afisa Uvuvi wa Halmashauri husika, Ofisi za Kanda za Sekta ya Uvuvi au tembelea **www.mifugouvuvi.go.tz**

Wananchi ambao wapotayari kukopa wawasilishe maombi yao Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Maombi yote yapitishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kabla ya kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kabla ya tarehe 29 Disemba, 2023 kupitia anuani ifuatayo;

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**
**S.L.P 2847**
**40487-DODOMA**
**Simu: +255 26 23 22613**
**Baruapepe: ps@uvuvi.go.tz**

# Shule mpya ya Kiboriani toka zama za hali mbaya

**Na Sanula Athanas, aliyekuwa** MPWAPWA

AGOSTI 7-11 mwaka jana, gazeti hili lilichapisha ripoti maalum kuhusu hali mbaya ya samani na miundombinu inayokinzana na mahitaji ya kitaaluma na kiafya katika Shule ya Msingi Kiboriani, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Habari hiyo ni zao la ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania iliyotolewa Machi 2017 na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Taasisi ya WAJIBU pia ilichukulia umuhimu mkubwa katika kujua undani wa yanayojitokeza shuleni Kiboriani na majirani zao - Shule ya Msingi Kikombo.

Katika ufuatiliaji huo, Nipashe ikijiunga kuwa sehemu ya walitaka ufumbuzi, ikidai ufafanuzi wa kiuchunguzi, ikaibua hali mbaya kuanzia madarasa na samani zake, madhila makubwa kwa vyoo vyake, walimu kutaabika kuanzia mazingira yao ya kazi - hawakuwa na ofisi, upungufu wa madarasa shuleni huku makazi yao yakiwa ni ya kujishikiza katika vibanda vilivyojengwa na wanakijiji kijijini huko.

Kimsingi, Kijiji cha Kiboriani kimejitenga mlimani umbali wa Km 13 kutoka mjini Mpwapwa, hakuna usafiri mwingine wowote isipokuwa pikipiki na mazingira ya safari yake husababisha umbali wake kufika Km 21 kutoka mjini unapozunguka kuupanda Mlima Kiboriani kiliko kijiji hicho. Kiko takribani Km mbili kutoka usawa wa bahari.

Baada ya ripoti hiyo ya Nipashe, kuliibuka mjadala toka kwa baadhi ya mamlaka za juu serikalini, huku baadhi zikikana kuwapo kwa ukweli huo.

Hata hivyo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kipindi hicho David Silinde, aliamua kuzuru shuleni Kiboriani kuthibitisha mwenyewe ukweli huo, akiambatana na mamlaka zinazohusika kuanzia wizarani hadi ngazi ya mkoa.

Hapo ndipo akakiri rasmi yote yaliyoripotiwa na Nipashe yalikuwa na ukweli, akitumia mtindo wa kile kilichoripotiwa gazetini anaoanisha na uhalisia alioshuhudia. Hiyo ilikuwa Agosti 9 mwaka jana.

Mara moja Naibu Waziri akakiri hali mbaya ya miundombinu na samani shuleni Kiboriani na akatoa ahadi ya serikali kutatua vikwazo vyote vilivyoshuhudiwa shuleni huko.

Serikali ikatoa kwa dharura Sh. milioni 195 kujenga miundombinu mipya shuleni. Pia ikatoa Sh. milioni 50 kumalizia mradi wa zahanati ulioanzishwa na wanakijiji.

ZAMANI

SASA





Maisha mapya ya makazi bora ya walimu ambao mwaka jana walikuwa wanahifadhiwa katika vibanda kijijini.





Vyoo bora vya kisasa shuleni Kiboriani kutoka hali mbaya iliyokuwapo miezi 14 iliyopita.

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA [MAHESABU YALIYO KAGULIWA]

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31-Dec-22 | Mwaka Uliopita 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 53,562 | 49,972 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 60,390 | 16,522 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 103,442 | 133,175 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 69,127 | 73,882 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 271 | 284 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 96,804 | 124,636 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 841,590 | 718,600 |
| 12 | Mali Nyingine | 43,162 | 41,047 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa<br>Haki ya matumizi ya mali | 20,610 | 22,599 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,288,958** | **1,180,715** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 862,393 | 738,724 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 124,778 | 178,978 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 2,207 | 3,967 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,780 | 1,502 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 2,641 | 8,362 |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,127 | 27,057 |
| 28 | Madeni | 129,401 | 108,912 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,172,328** | **1,067,502** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **116,631** | **113,213** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 28,072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 72,411 | 65,567 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,154 | 9,141 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 10,433 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **116,631** | **113,213** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 151,019 | 207,028 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 72,800 | 80,859 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,323 | 15,554 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 244 | 11 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.05% | 9.59% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.43% | 10.94% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 87.44% | 80.52% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.29% | 69.20% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.83% | 82.70% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 7.57% | 14.27% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9.17% | 13.13% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Limbikizo la Mwaka Mwaka Wa Sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 139,782 | 135,178 |
| 2 | Gharama za Riba | (48,570) | (39,787) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **91,213** | **95,391** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | **(1,758)** | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (13,945) | (13,669) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **32,818** | **34,506** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na miamala ya Fedha za Kigeni | 4,138 | 2,246 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 19,352 | 26,021 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 9,328 | 6,238 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(101,457)** | **(96,563)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 49,806 | 50,912 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 9,174 | 581 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 42,478 | 45,070 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **6,871** | **19,665** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 3,717 | 10,498 |
| 10 | **Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,154** | **9,167** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **630** | **(253)** |
| | 11.1 Hasara ya sasa kutoka kwa wajibu wa faida | 901 | (362) |
| | 11.2 Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (270) | 108 |
| | 11.3 Gharama ya zamani juu ya wajibu wa faida | - | - |
| | 11.4 Kodi iliyopungua kwa gharama ya zamani kwenye wajibu | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **3,784** | **8,914** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 1,086 | 1,091 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 101 | 326 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 48 | 47 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.25% | 0.75% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.70% | 7.87% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 58.78% | 74.34% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8.95% | 9.77% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 6,871 | 19,665 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 25,966 | 13,913 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (136,740) | (102,603) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | 4 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 82,874 | 114,617 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (50,046) | (22,531) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,195 | (12,704) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (235) | 2,505 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (9,459) | (7,800) |
| | - Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (618) | (529) |
| | - Gharama ya mafao ya mtumishi | 1,766 | 1,137 |
| | - Mengineyo (Mapato ya ruzuku & hifadhi nyingine) kutoka muunganiko wa | (229) | 85 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(76,655)*** | ***5,759*** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,330) | (7,709) |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoonekana | (577) | (855) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | ***(2,907)*** | ***(8,563)*** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Fedha Taslimu iliyolipwa kwenye kodi ya share za bonasi | (367) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Malipo ya Dhima ya Kukodisha | (6,151) | (6,791) |
| | Mengineyo (Kodi katika Hisa za Ziada & Ruzuku Iliyopokelewa) | 93 | 267 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***(6,425)*** | ***(6,524)*** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(85,987)** | **(9,329)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 111,197 | 120,526 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **25,211** | **111,197** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mafao yanayoelezeka | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **77,600** | **(2,891)** | **739** | **-** | **9,694** | **113,213** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,154 | | - | - | - | **3,154** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 630 | | - | - | - | **630** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 739 | | (739) | - | - | - |
| Fedha Taslimu iliyolipwa kwenye kodi ya share | - | - | (367) | | - | - | - | **(367)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa baada | - | - | - | | - | - | - | - |
| Kurudishwa kwa Gawio lililosimamishwa | 3,300 | - | (3,300) | | - | - | - | **0** |
| Mengineyo | - | - | - | | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | **-** | **78,456** | **(2,891)** | **-** | **-** | **9,694** | **116,631** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **69,172** | **(2,638)** | **-** | **-** | **9,694** | **104,299** |
| **Mabadiliko ya IFRS 9** | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 9,167 | (253) | - | - | - | **8,914** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (739) | | 739 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | | - | - | - | - |
| **Gawio lililolipwa** | - | - | - | | - | - | - | - |
| faida ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hamisho kutoka/kwenda hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | **28,072** | **-** | **77,600** | **(2,891)** | **739** | **-** | **9,694** | **113,213** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2022

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **MR.S.K.MOSHINGI**<br>**Afisa Mtendaji mkuu** | **Imesainiwa** | **09.10.2023** |
| **MS. REGINA E. SEMAKAFU**<br>Mkuu wa Fedha | **Imesainiwa** | **09.10.2023** |
| **MR. S.NYENYEMBE**<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | **Imesainiwa** | **09.10.2023** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA**<br>Mwenyekiti wa Bodi | **Imesainiwa** | **09.10.2023** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI**<br>Mjumbe wa Bodi | **Imesainiwa** | **09.10.2023** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# AFL itumike kuonesha Tanzania inastahili mechi ya fainali Afcon

**IJUMAA** wiki hii Klabu ya Simba itaikaribisha Al Ahly ya Misri katika mchezo wa ufunguzi wa michuano mipya ya African Super League (AFL), utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika michuano hiyo inayoshirikisha Klabu nane bora zaidi barani Afrika, ambazo ni Al Ahly (Misri), Enyimba FC (Nigeria), Esperance Tunis (Tunisia), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Petro Atletico de Luanda (Angola), Simba (Tanzania), TP Mazembe (DR Congo) na Wydad Casablanca (Morocco), na itachezwa kwa mtindo wa mtoano nyumbani na ugenini huku Tanzania ikipewa fursa ya mchezo wa ufunguzi kupigwa hapa nchini.

Tayari maandalizi kabambe yamefanyika na yanaendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Benjamin Mkapa uliofanywa kwa ushirikiano wa serikali, Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) na lile la Afrika, CAF.

Hii ni michuano mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu Afrika huku CAF na Fifa wakiipa hadhi ya juu, hivyo pamoja na maandalizi makubwa yaliyofanywa na Klabu ya Simba na serikali, ni wakati sasa kwa mashabiki wa soka, wadau na Watanzania kwa ujumla kwenda uwanjani kuiheshimisha Tanzania.

Haitakuwa na maana kufanyika maandalizi yote hayo halafu siku ya tukio kuishia kuitazama mechi hiyo ya ufunguzi kupitia televisheni kwa kuwa 'shughuli ni watu', hivyo ununuzi wa tiketi unapaswa kufanyika kwa wingi kwenda kuujaza Uwanja wa Mkapa.

Si hilo tu, bali pia pamoja na uwanja kujaa tunataka kuona 'vaibu' ya mashabiki wakishangilia mwanzo mwisho ili kunogesha mchezo huo na kuipa hamasa Simba ili kupata ushindi.

Kadhalika, ni wakati wa kuweka itikadi zetu za kiklabu pembeni na wote kuwa kitu kimoja kwa kuisapoti Simba Ijumaa, kwani Simba ikishinda 'Tanzania imeshinda' kwa kuwa soka letu litazidi kuwa katika daraja la juu.

Pamoja na hayo yote, jambo lingine la muhimu kwa mashabiki wanapaswa kuwa wastarabu kwa kushangilia kwa 'fujo zisoumiza' na kutumia miundoumbinu ya uwanja kistaarabu zaidi ili kuzidi kuvutia michuano mingine mikubwa ama mechi za ufunguzi na za fainali kuletwa hapa nchini.

Tunatambua huwa kuna baadhi ya mashabiki wanakosa ustaarabu hususan vyooni wanapomaliza haja zao huona tabu kuruhusu maji ya kuondoa uchafu, mambo ambayo hatutarajii kuyaona Ijumaa uwanjani hapo kutokana na ukubwa wa tukio lenyewe na uwapo wa ugeni mkubwa.


Lingine ni kwa wasimamizi wa uwanja huo kuhakikisha yanakuwapo maji ya kutosha vyooni kwani mara kadhaa pia wakati wa mechi uhaba huo umekuwa ukijitokeza siku za nyuma.

Tunataka kuona mechi bora ya ufunguzi kuanzia nje hadi ndani ya uwanja ikienda sambamba na sapoti kubwa kwa Simba kupata matokeo ili katika mchezo huo na hata ule wa marudiano Oktoba 24, mwaka huu, kufanikiwa kusonga mbele.

Tunaamini tukionesha mechi ya ufunguzi bora iliyokamilika, itasaidia kuishawishi CAF kuelekea fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, ambazo zitafanyika Afrika Mashariki kwa ushirikiano wa Tanzania, Kenya na Uganda, tunaweza kupewa nafasi ya mchezo wa ufunguzi na hata ule wa fainali kupigwa nchini.

Hivyo, hii ni fursa kwa kila mmoja kuwania nafasi hiyo ya kwenda kwa Mkapa kuiheshimisha nchi bila kujali itikadi za kiklabu, lakini pia uungwana na ustarabu wa hali ya juu ukitawala ili kuonesha kweli Tanzania ni mahali salama zaidi kwa wageni na burudani ya soka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Taifa Stars ikikaza inaweza kutoboa makundi AFCON

Na Adam Fungamwango

**BAADHI** ya Watanzania wameanza kuwa na wasiwasi baada ya kumalizika droo ya upangwaji wa timu zitakazocheza fainali za Mataifa ya Afrika AFCON 2023 yatakayochezwa mwakani kuanzia Januari 13 hadi Februari 11 nchini Ivory Coast. Tanzania imeangukia Kundi F ambalo pia lina timu za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Zambia na Morocco. Kinachowatia hofu kwanza kabisa ni historia ya timu hizo, kwani zote zimeshawahi kuutwaa ubingwa wa Afrika kasoro Taifa Stars tu.

Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ilitwaa ubingwa huo mara mbili mwaka 1968 na 1974, Morocco mara moja 1976, na Zambia iliubeba nchini Gabon mwaka 2012.

Timu inayoogopwa zaidi na Watanzania wengi ni Morocco hasa ushiriki wake mwaka jana kwenye Kombe la Dunia ambapo kwa mara ya kwanza ilivunja mwiko wa Waafrika kuishia hatua ya robo fainali ya michuano hiyo na kuifunga Ureno bao 1-0, kabla ya kutolewa kwenye hatua ya nusu fainali kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Ufaransa.

Ukiwasikiliza Watanzania wengi, hata baadhi ya makocha, achilia mbali wachambuzi ni kwamba Morocco tayari wameipa nafasi ya kwanza katika kundi hilo.

Wakabainisha kuwa Stars kama inataka kusonga mbele kwenye kundi hilo, inatakiwa kupambana na Zambia na DR Congo kugombea nafasi ya pili ili kuipata robo fainali.

Sasa wapo ambao pia wanazihofia hata Zambia na DR Congo wakidai ni kweli katika miaka ya karibuni zilishuka kimpira, lakini zinaonekana kurejea kwa kasi na zikionekana zipo juu, hivyo kuwa na wasiwasi na timu ya Tanzania.

Hata hivyo, Watanzania wakumbuke kuwa hili si kundi la kusaka tiketi ya kusaka kuingia makundi, bali ni kundi la kusaka ubingwa wa Afrika. Kwa maana hiyo huwezi kukutana na timu nyepesi au taifa ambalo lipo nyuma kisoka kwa sababu mbalimbali.

Kwenye hatua hii huwezi kukutana na kundi la timu kama Djibouti na Somalia, bali timu ambazo zimepambana na kutinga makundi.

Ni kama Ligi ya Mabingwa tu, huko ni lazima ukutane na kina Al Ahly, Wydad, Esperance, Mamelodi Sundowns na hakuna namna kama unaingia hatua ya makundi ya ligi hiyo ukawakosa. Ukizikosa kwenye kundi utakutana nazo robo fainali, nusu, au fainali.

Ndivyo ilivyo hata kwenye AFCON, haipaswi kuihofia timu yoyote kwa sababu kama Stars itatoboa huko mbele itakutana na timu ngumu zaidi. Binafsi naona Watanzania kwa sasa tumeshatoka huko kwenye kuzihofia timu iwe za klabu au za taifa.

Stars ilipata tiketi ya kucheza AFCON ugenini ikivimbia moja ya timu kubwa Afrika, Algeria na kutoka suluhu, hivyo sidhani kama kuna woga tena.

Wachezaji wetu hawana woga tena kwa sababu baadhi ya wachezaji wa timu zingine za taifa wapo nao kwenye klabu moja mfano kina Fiston Mayele na Henock Inonga wa DR Congo na Clatous Chama wa Zambia, au wameshawahi kukutana nao katika mechi za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Simba imetinga robo fainali mara nne mechi za kimataifa na Yanga fainali ya Kombe la Shirikisho, sidhani kama wachezaji wake wa Kitanzania watakuwa na hofu tena au kuliona eti kundi ni gumu.

Tanzania kwa sasa pia ina wachezaji kadhaa wanaocheza soka la kulipwa nje akiwamo Dismas Novatus wa Klabu ya Shakhtar Donetsk ya Ukraine na wenzake, hivyo kama baadhi ya hawajui Taifa Stars kwa sasa ni moja kati ya timu zinazokuja juu kisoka Afrika.

Ni kwa sababu ya kuwa na ligi bora, wachezaji wakubwa kuja kucheza hapa nchini na kuwapa changamoto wazawa, kiasi baadhi yao sasa kutoka kwenda nje ya nchi, akiwamo Baraka Majogolo anayekipiga Chippa United ya Afrika Kusini.

Binfasi, naona kama Stars ikijipanga tu vizuri, itafanya vema na kufanikiwa kupita kwenye hatua hii licha ya kuonekana kama kundi ni gumu.

# Wananchi milioni 24 wasajiliwa kupata vitambulisho vya NIDA

**Na Samson Chacha,** MARA

WANANCHI milioni 24 wamesajiliwa katika mpango wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) huku Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akiwahimiza viongozi wa vijiji na mitaa kutoa ushirikiano kwa maofisa wa NIDA wakati wa ugawaji vitambulisho hivyo.

Aliyasema hayo katika uzinduzi wa ugawaji vitambulisho vya NIDA uliofanyika mwishoni mwa wiki, Musoma mkoani Mara.

Masauni aliongozana na Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Ismail Bumatila, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda na viongozi wa serikali na maofisa wa mamlaka hiyo wa wilaya sita za mkoa huo.

"Tunazindua kitaifa ugawaji wa vitambulisho vya NIDA hapa Musoma, Wizara ya Mambo ya Ndani tunawahimiza viongozi wa vijiji na mitaa kote nchini kutoa ushirikiano kwa maofisa wetu wakati watakapofika katika maeneo yao kugawa vitambulisho hivi na kama kuna kasoro ama tatizo watoe taarifa kwa wahusika ili kutatua tatizo litakalojitokeza katika ugawaji.

"Zoezi hili la kugawa vitambulisho linatarajiwa kuanza wakati wowote ule na vina umuhimu mkubwa kwa wananchi wetu ukiwamo kupata huduma za maendeleo na kuwa makini na watu wasio raia kujipatia vitambulisho hivyo kinyume na utaratibu na kwa maofisa wa NIDA kuepuka vitendo vya rushwa na wananchi watoe taarifa kwa vyombo husika kwa watumishi wanao waomba rushwa ili wapatiwe vitambulisho hivyo," alisema Waziri Masauni.

Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Bumatila alisema wananchi milioni 24 wamesajili kupatiwa vitambulisho vya taifa na serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani imejipanga kufikia Desemba 2023, wananchi waliosajiliwa watakuwa wamepatiwa vitambulisho vya taifa.

"NIDA imeongeza kasi ya uzalishaji wa vitambulisho hivyo na vyenye ubora zaidi na tunatarajia kuvisambaza na kuvigawa kote nchini tunaomba ushirikiano kutoka kwa viongozi hao wa vitongoji, vijiji na mitaa na wananchi wenyewe ili zoezi liweze kufanikiwa kwa asilimia 100," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda alisema, maofisa wa NIDA wanatakiwa kuvigawa vitambulisho hivyo kwa wananchi ambao ni Watanzania bila vikwazo. "Tunaonya maofisa wa NIDA watakaohusika katika zoezi la ugawaji vitambulisho hivyo kuepuka vitendo vya rushwa wakiwamo viongozi wa vijiji na mitaa kwa kuwa rushwa ni adui wa haki na kutokana na rushwa watu wasio raia wanaweza kujipenyeza kupata vitambulisho hivyo kinyume na utaratibu," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo (kushoto), akipongezwa na Mkuu wa Idara ya Biashara wa Benki ya NMB, Alex Mgeni (katikati), baada ya kutoa hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, wakati wa Jukwaa la Wafanyabiashara Wakubwa Kanda ya Dar es Salaam wanaohudumiwa na benki hiyo, lililofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Kariakoo, William Nkuna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ajivunia kusisimua uchumi, CRDB ikifungua tawi Kwimba

**Na Mwandishi Wetu,** NKWIMBA

MKUU wa Wilaya ya Kwimba, Ng'wilabuza Ludigija, amesema kufunguliwa tawi la Benki ya CRDB wilayani humo kutasisimua zaidi uchumi wa halmashauri na wananchi wake.

Ludigija amesema wengi wanaufahamu Mkoa wa Mwanza umebarikiwa kwa fursa nyingi za uchumi kuanzia madini, uvuvi, kilimo na hata utalii, hivyo kuwapo taasisi za fedha kama Benki ya CRDB kunaongeza kujiamini kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kutekeleza mipango yao wakiwa na uhakika wa usalama wa fedha zao.

"Sio tu kwamba Mwanza inajitegemea kwa chakula, bali pia inaingiza fedha nyingi za kigeni kutokana na kilimo cha pamba, uvuvi, utalii na usafirishaji, hivyo kuzivuta taasisi za fedha ndani ya halmashauri zake na sasa Kwimba hatuna sababu ya kujiuliza kuhusu mikopo na usalama wa fedha zetu.

"Tuitumie mikopo inayotolewa na Benki ya CRDB kutekeleza miradi yetu ili kuinua kipato cha kila mmoja wetu na uchumi wa halmashauri yetu kwa ujumla," alisema Ludigija jana alipozindua tawi la Benki ya CRDB lililoko Ngudu, wilayani Nkwimba.

Kwimba ni moja ya halmashauri saba zinazounda Mkoa wa Mwanza yenye fursa nyingi zinazoweza kuwanufaisha wananchi iwapo watapata mtaji wa kuziongezea thamani malighafi zilizopo.

"Kwa tawi hili la Benki ya CRDB linalofunguliwa leo (jana) hapa Ngudu, linaifanya Benki ya CRDB kufikisha matawi 18 katika Mkoa wa Mwanza. Hii ni idadi kubwa ya matawi kwa taasisi moja ya fedha kuwa nayo katika mkoa mmoja.

"Wananchi wengi wa wilaya hii wanajihusisha na kilimo kinachowahikikishia upatikanaji chakula na kuwaingizia kipato, hivyo kukidhi vigezo vya kupata huduma za kibenki. Ni matumaini yangu kuwa watachangamkia fursa," alisema Ludigija.

Kiongozi huyo alikumbusha wananchi kwamba huduma za benki ni muhimu na elimu yake inapaswa kufundishwa kwa watoto tangu wakiwa wadogo ili kuwapa maarifa muhimu yatakayowasaidia kufanikisha malengo yao ya kiuchumi pindi watakapokuwa wakubwa.

Hata kwa watu wazima, Ludigija alisema elimu ya fedha ni muhimu na huduma za benki zinapaswa kuwa kipaumbele cha kila mmoja.

"Kufunguliwa kwa tawi hili kutaongeza tija iwapo wakulima wengi zaidi watapata mikopo inayotolewa na Benki ya CRDB, tena kwa riba ndogo ya chini ya asilimia 10.

"Serikali imejitahidi kujenga vituo vya afya vinavyotoa huduma za uhakika na halmashauri inashirikiana na vikundi vya wanawake na vijana wanaoweza kunufaika na programu ya Imbeju inayotoa mtaji wezeshi.

"Iwapo fursa za Imbeju zitachangamkiwa na wana Kwimba, hakika huu utakuwa mwaka unaoweka msingi wa mafanikio ya kiuchumi kwa wengi," alisema.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Mikopo wa Benki ya CRDB, Xavery Makwi alisema kwa miaka 27 tangu kuanzishwa kwake, benki hiyo imekua na kutanua mtandao wake wa huduma kutoka matawi 19 yaliyokuwapo mwaka 1996 mpaka matawi 261 sasa hivi, hivyo kuenea katika halmashauri zote nchini.

Ukuaji huo, Makwi alisema unaakisi malengo yao ya kusogeza huduma karibu na Watanzania bila kujali wanaishi mjini au kijijini.

Licha ya idadi kubwa ya matawi waliyonayo, alisema Benki ya CRDB imekuwa ikibuni na kuingiza sokoni njia mbadala zinazorahisisha ufikishaji huduma kwa wateja zinazojumuisha mawakala zaidi ya 25,000 na mashine za kutolea fedha (ATM) zaidi ya 550.

"Hii ndio maana halisi ya kaulimbiu yetu ya 'Ulipo Tupo'. Ninajivunia kukujulisha kupitia njia hizi mbadala za ufikishaji wa huduma, benki yetu imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza ujumuishi wa kifedha kwa wananchi," alitamba.

Wilayani Kwimba, Makwi alisema wanao mawakala 26 ambao ni sehemu ya 1,500 wanaohudumia mkoa mzima wa Mwanza, hivyo akawasisitiza wananchi kuyatumia majukwaa yaliyopo kukidhi mahitaji yao ya kifedha kwa kuwa sasa hivi Benki ya CRDB inajali hata imani za kidini.

"Tunalo dirisha la Al Barakah Banking maalumu kwa wateja ambao wangependa kupata huduma zinazofuata misingi ya sharia ya dini ya Kiislam," alisema.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Shule yakabiliwa uchakavu majiko, sufuria

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHULE ya Sekondari ya Wavulana ya Kibaha inakabiliwa na kikwazo cha uchakavu wa majiko ya gesi yanayotumika kupikia chakula cha wanafunzi.

Kati ya majiko sita yaliyopo, manne ni chakavu na hayawezi kurekebishika kutokana na kutumika kwa muda mrefu tangu shule hiyo ilipoanzishwa.

Hayo yamebainishwa katika risala iliyosomwa na mwanafunzi, Gration Sangeda, kwenye mahafali yaliyofanyika mwishoni mwa wiki katika shule hiyo inayomilikiwa na Shirika la Elimu Kibaha.

Wanafunzi hao pia walibainisha uchakavu wa masufuria ya kupikia na kwamba yaliyopo yanahitaji ukarabati ili yaweze kuendana na muda wa chakula kwa wanafunzi kuwahi vipindi vya darasani.

Kwa mujibu wa risala hiyo sufuria moja la chakula linauzwa Shilingi milioni tatu, yaliyopo wamekuwa wakiyaziba mara kwa mara na endapo masufuria hayo yatanunuliwa mapya yatarahisisha chakula kupikwa kwa wakati na kuwezesha wanafunzi kuwahi vipindi vya darasani.

Kadhalika, walielezea uchakavu wa mfumo wa vyoo ambao hauridhishi kwa sasa na unahitaji marekebisho kwa kuwa mabomba yaliyopo ni ya chuma na yamekuwapo kwa miaka zaidi ya 30 tangu shule hiyo ianzishwe.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kibaha, George Kazi aliishukuru Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) kwa kusaidia uchimbaji wa kisima kilichogharimu zaidi ya Sh. milioni 64 na kumaliza kikwazo cha maji kilichokuwapo awali.

Alisema kupitia kisima hicho shule itaanzisha bustani za mboga ambazo zitakuwa zinatumika shuleni kuimarisha afya za wanafunzi.

Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe, alimwomba Mkuu wa shule kuwashirikisha waliosoma katika shule hiyo kukutana na kufanya nao mawasiliano ili waweze kutatua vikwazo vya jiko na sufuria zinazohitajika.

Vilevile, Mbalwe alisema kupitia maji ambayo kwasasa yanapatikana kwa uhakika shule hiyo inatakiwa kuanzisha bustani ya miti na kuanzisha maeneo rasmi ya miti kuwa ya mfano kwa kutunza mazingira.

Kabla ya kuchimbwa kisima katika shule hiyo wanafunzi walikuwa wanatumia muda mwingi kwenda kufuata maji nje ya shule na wakati mwingine kukosa masomo.

# Mshomba: NSSF ni wadau muhimu kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amepongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kuwawezesha na kuwainua vijana kupata fursa za ajira.

Mshomba amesema hayo mwishoni mwa wiki, wakati alipotembelea Maonesho ya Wiki ya Vijana yanayofanyika katika stendi ya zamani, Babati mkoani Manyara, akiwa amefuatana na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa NSSF, Omar Mziya na Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani, Godfrey Ngonyani.

Amempongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha vijana wanashiriki shughuli mbalimbali za kiuchumi.

"Namtakia kila la heri Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha malengo yake aliyonayo kwa vijana na Watanzania kwa ujumla yanatimia na nchi yetu inapiga hatua za maendeleo," alisema Mshomba.



Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, akipata maelezo kutoka kwa Ofisa TEHAMA wa NSSF, Nuru Mbeyu.

Mshomba alisema vijana ni wadau muhimu kwa NSSF kwa sababu ndio nguvu kazi kubwa ya taifa, na pia ni wanachama wa Mfuko, ambao baadhi wanachangia kupitia sekta binafsi na wengine kupitia sekta isiyo rasmi.

"Ushiriki wa NSSF katika maonesho haya ya Wiki ya Vijana, umewalenga moja kwa moja vijana ambao tunawapatia elimu ya hifadhi ya jamii ili waweze kujiunga na kujiwekea akiba kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye," alisema Mshomba.

Alisema suala la hifadhi ya jamii ni muhimu kwa sababu linatoa uhakika wa maisha ya binadamu hasa baada ya uwezo wake wa kufanyakazi kupungua na NSSF itamlipa mafao yakiwamo ya uzee.

Mshomba alitoa wito kwa wananchi wakiwamo vijana kujiunga na kuchangia kwa wingi ili kuandaa kesho yao iliyokuwa njema.

Alipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa walivyojipanga vizuri na kufanikisha maadhimisho hayo.

Vilevile, ameipongeza Bodi ya Wadhamini kwa miongozo wanayotoa kwa NSSF pia wafanyakazi kwa kazi nzuri wanazofanya.

Alisema NSSF iko imara na mpango wa uchangiaji wa sekta isiyo rasmi uko imara na lengo ni kuhakikisha inawafikia wananchi wengi zaidi kupata elimu ya hifadhi ya jamii pamoja kuwaandikisha kwa ajili ya kujiwekea akiba.

# 'Wazazi simameni kikamilifu katika malezi ya watoto'

**Na Denis Mambya,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA), Manispaa ya Morogoro, Shekhe Habib Salim Mwenge, ameiomba jamii kuwa mstari wa mbele katika malezi itakayowawezesha watoto kukua katika maadili mema na yenye kumpendeza mwenyezi Mungu na jamii kwa ujumla.

Shekhe Habib alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu wazazi kuacha jukumu la ulezi wa watoto kwa wasaidizi wa kazi na katika vituo vya kulelea watoto (Day Care) jambo linalosababisha kukosa malezi bora

Kadhalika alisema, wazazi wanatakiwa kuwa waangalifu katika malezi ili kuepusha vitendo viovu dhidi ya watoto ukiwamo ukatili, ambao hufanywa na wasaidizi wa kazi ama katika vituo vya kulelea watoto, kutokana na visa vingi vya ukatili kuripotiwa.

''Mzazi anapoacha jukumu la ulezi wa mtoto katika vituo au kwa wasaidizi wa kazi husababisha mtoto kukosa maadili bora, kutokana na kuiga tabia na mienendo mibovu kulingana na mazingira ambayo mzazi humwacha mtoto," alisema Shehk Habib. Cosmas Kigona, Mratibu wa Parokia ya Mtakatifu Patrick Jimbo la Morogoro, alisema wazazi wengi wamesahau jukumu lao la msingi la ulezi wa watoto, kwa kuwa siyo sahihi kumwacha mtoto mwenye umri mdogo katika vituo vya kulelea na kwamba ni vyema wakasimama kikamilifu katika nafasi ya malezi.

"Kuna muda mzazi huacha jukumu la ulezi kwa msaidizi wa kazi pasipo kutambua tabia, mwenendo wa msaidizi huyo na mazingira aliyotoka, kwani huweza kusababisha makuzi yasiyo sahihi kwa mtoto husika," alisema Cosmas Kigona.

Othman Shariff, Mkazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, alitaja sababu inayowafanya wazazi kutokutimiza jukumu la malezi kwa watoto ni kutotambua athari zinazowakumba watoto wawapo katika vituo vya kulelea.

## TANGAZO LA MNADA

Held auctioneer, EIE ,Synarge company na Cops Auction Mart Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari na Nyumba Mjini Dar es salaam Dodoma na Bagamoyo Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Ernest Nyasenso Ikwabe | TOYOTA HIACE -T811DMP ipo Dodoma | 28.10.2023 |
| Mwamini Livingstone Mzuzu | TOYOTA COASTER -T449AAC ipo Dodoma | 28.10.2023 |
| Hezron Aidan Magawa | TOYOTA COASTER -T197BBH Ipo Dodoma | 28.10.2023 |
| Lydia John Maganga | House located At Msigani-Ubungo | 28.10.2023 |
| Wilson Salvatory Lyembela | TOYOTA ALTEZZA-T272 DDG | 28.10.2023 |
| Lydia Gabriel Laswai | Plot of land located at Ukuni-Bagamoyo | 28.10.2023 |
| DANIEL VICENT KADUDU | Home chattels located at Madale | 28.10.2023 |
| Athumani Juma Malole | TOYOTA COASTER T188BLK | 28.10.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano piga 0655319097(cops),0657384471(EIE) au 0677014355(Fanikiwa) 0713197485(Held auctioneer) 0745744744(Synarge)**

TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LIMITED

## PUBLIC NOTICE



JOSEPH FREDY SARIA

We would like to inform our stakeholders and the general public that **Joseph Fredy Saria** is no longer employed with Tujijenge Tanzania Financial Services Limited.

For official communication with Tujijenge Tanzania Financial Services please contact **+255 739 611 611 / +255 739 611 612**

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KINONDONI
MWANANYAMALA
SHAURI LA MADAI NAMBARI 447 LA 2023
DR. HAMZA MUGULA......MUOMBAJI/WAOMBAJI
DHIDI YA
01.MASTER CLASS WORLD WIDE LTD
02.PAUL MASHAURI MDAIWA/WADAIWA
03.LEONIDA BARONGO

**WITO KUITWA SHAURINI**

01. MASTER CLASS WORLD WIDE LTD
02. PAUL MASHAURI
03.LEONIDA BARONGO

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

DR. HAMZA MUGULA Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 02/11/2023 saa 3:00AM Asubuhi mbele ya J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 Mwezi 10 , 2023

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.97 OF 2023
IN the Matter of the late:MARIA JACKSON

By 1.LUCIA JACKSON MANDWEKE
2.............................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 17 October 2023.

**Dated at Morogoro this 09 day of October 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

# MATANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

### ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Mthamini Mkuu wa Serikali ameshaidhinisha jedwali la fidia lililozingatia maoni yake na wadau wengine, na sasa zoezi la ulipaji fidia linatarajiwa kuanza mapema iwezekanavyo. Ikumbukwe kuwa jedwali hili la fidia linawahusu waathirika wa mradi walioafiki fidia zao wakati wa zoezi la kuhakiki fidia lililofanyika mwezi Machi 2023.

Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo ya fidia pamoja na kuhakiki taarifa za benki kabla ya kufanya malipo. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata kwa ratiba ifuatayo:

| Eneo la Usainishwaji | Kata | Mitaa Inayohusika | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 18 hadi 20/10/2023 |
| | | Misheni Kota | 21 na 22/10/2023 |
| | | Ilala Kota | |
| | Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| | Upanga Magharibi | Charambe | 31/10/2023 hadi 02/11/2023 |
| | Jangwani | Mtambani A | |
| | | Mtambani B | |
| | | Jangwani | |
| Ofisi ya Kata - Magomeni | Magomeni | Suna | 23 hadi 25/10/2023 |
| Ofisi ya Kata - Mzimuni | Mzimuni | Idrisa | 26/10/2023 |
| | | Mtambani | |
| | | Mwinyi Mkuu | |
| Shule ya Msingi Mapinduzi - Kigogo | Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 27 na 28/10/2023 |
| | Hananasif | Mkunguni A | 29 na 30/10/2023 |
| | | Mkunguni B | |
| | | Hananasif | |
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | | Kawawa | 3 hadi 5/11/2-23 |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

TANGAZO KWA UMMA

### ZOEZI LA UHAKIKI WA MALI ZILIZOATHIRIKA NA MRADI KWA WATU AMBAO HAWAKUAFIKI VIWANGO VYA FIDIA NA WALIOSAJILI MALALAMIKO

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Kufuatia zoezi la uhakiki wa fidia lililofanyika mwezi Machi 2023, baadhi ya waathirika wa mradi hawakuafiki viwango vya fidia walivyo onyeshwa, na baadhi walisaini kuridhia viwango vya fidia na kisha kuandika barua za malalamiko. Katika kushughulikia malalamiko yao, OR-TAMISEMI inatarajia kufanya zoezi la kuhakiki upya mali za waathirika hao kwa kuzingatia aina ya malalamiko yao. Kutakuwa na timu mbili za wathamini kwa wilaya za Kinondoni na Ilala ambazo zitapita kwenye makazi ya waathirika husika kwa ratiba ifuatayo:

| Tarehe | Mtaa Itakayotembelewa | |
|---|---|---|
| | Timu ya Ilala | Timu ya Kinondoni |
| 19 na 20/10/2023 | Msimbazi Bondeni | Kigogo Mbuyuni |
| 23 na 24/10/2023 | Charambe | Hananasif |
| | Ilala Kota | Mkunguni A |
| | Mtambani A | Mkunguni B |
| | Mtambani B | Idrisa |
| | Kariakoo Kaskazini | Suna |
| | | Mwinyimkuu |

Wahusika wanaombwa kutoa ushirikiano kwa kuwepo katika ofisi za Serikali za Mitaa yao kuanzia saa 2:00 asubuhi.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

MAZUNGUMZO MAALUM -3

# Simulizi za Kimiti vita uhujumu uchumi

Na Mwandishi Wetu

KATIKA utawala wa awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere, taifa lilikumbwa na uhaba wa bidhaa muhimu kwa mahitaji ya kila siku. Hali hiyo ilisababisha ulanguzi kutamalaki na bidhaa nyingi kuuzwa kwa magendo.

Kutokana na hatua hiyo, serikali ilianzisha vita dhidi ya ulanguzi na uhujumu uchumi iliyoongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, wakati huo ikiwa chini ya Edward Moringe Sokoine. Mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti, ambaye wakati wa vita hivyo miaka ya 1980 alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu akishughulikia Serikali za Mitaa na Vyama vya Ushirika, anasimulia hali ilivyokuwa na hatua zilizochukuliwa na serikali.

Kimiti anasema baada ya vita vya Uganda mwaka 1978/79, hali ya uchumi ilikuwa mbaya. Kulikuwa na ukosefu wa bidhaa mbalimbali na ulanguzi ulikuwa juu. Hatua hiyo pia ilisababisha mapato ya serikal kupungua, hivyo serikali ilichukua hatua za kukabiliana na hali hiyo.



Paul Kimiti,

"Nakumbuka wakati ule serikali ilipotangaza vita dhidi ya ulanguzi na uhujumu uchumi, Sokoine akiwa Waziri Mkuu, alikuwa na mawaziri wa nchi watatu, mimi nikishughulikia serikali za mitaa na vyama vya ushirika, Gertude Mongela (Tawala za Mikoa) na Anne Makinda (Sera na Uchumi). Wote tulipewa jukumu la kumsaidia Sokoine kuhakikisha tunafanikiwa katika vita hivi.

"Vita dhidi ya uhujumu uchumi ilipamba moto. Kutokana na unyeti wa vita hivyo, iliamuriwa kuwa mawaziri wote tuliokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu wapewe ulinzi.

Watu walifikiri tumehusika kuwakamata watuhumiwa wa magendo na uhujumu uchumi. Ma- RPC (makamanda wa polisi wa mikoa) baadhi yao nao walitiwa ndani.

"Haikuwa kazi rahisi lakini tulifanikiwa kwa kiasi kikubwa. Muda mfupi baada ya kuanza kushughulikia suala hili, kulianza kuwa na unafuu wa upatikanaji wa bidhaa," anasema.

**HATUA ZA SERIKALI**

Katika kuhakikisha vita dhidi ya ulanguzi wa bidhaa na uhujumu uchumi vinafanikiwa, Kimiti anasema serikali ilichukua hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza, anasema serikali ilitunga Sheria ya Uhujumu Uchumi na kupitia sheria hiyo, watu waliobainika kufanya magendo na kuwahujumu wananchi, walichukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria.

"Wako wafanyabiashara waliofikishwa katika vyombo vya sheria na wengine walifungwa. Viongozi wa serikali katika ngazi mbalimbali waliobainika kushiriki katika vitendo hivyo, nao walijibishwa.

"Sheria ya ulanguzi ilisaidia sana watu kuwa waoga kuwadhulumu wengine. Hakuna aliyeonewa huruma. Ukibainika umefanya kosa hilo wewe ni kufikishwa kwenye vyombo vya sheria au kuwajibishwa na hatimaye sharia kuchukua nafasi yake," anabainisha.

Hatua ya pili iliyochukuliwa na serikali, kwa mujibu wa Kimiti, ni kuanzishwa kwa kampuni za biashara za mikoa (RTC) ili kudhibiti magendo na bei za ulanguzi wa bidhaa.

Anasema bei katika maduka yote ya RTC kwenye mikoa yote zilikuwa zinafanana. pia anasema serikali pia ilianzisha sera za bei na mishahara kwa lengo la kudhibiti mianya ya ukosefu wa bidhaa.

Kimiti pia anasema kipindi hicho wafanyabiashara wengi walificha fedha na wengine wakawa wanazitupa holela. Ili kudhibiti hali hiyo, anasema serikali ilianzisha mpango wa kubadili fedha kwa kuziondoa noti za Sh. 100 zilizokuwa maarufu kwa jina la Masai ili fedha zirudi kwenye mzunguko.

Sambamba na hatua hizo, Kimiti anasema mwaka 1983, serikali ilitoa Waraka Namba Moja wa 1983 wa Vita vya Taifa vya Uchumi na Kazi Muhimu za Serikali Mpya ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Waraka huo pamoja na mambo mengine ulisisitiza umuhimu wa watu kufanya kazi na uwajibikaji kwa viongozi. Anasema waraka huo ndio uliotumiwa na serikali, Sokoine akiwa Waziri Mkuu na kwamba kiongozi huyo anafuatilia utekelezaji na alikuwa na msimamo katika mambo mbalimbali.

**UKOSEFU MAFUTA**

Moja ya bidhaa ambazo zilipatikana kwa shida wakati wa ulanguzi na uhujumu uchumi ni mafuta. Kimiti anasema kuna wakati taifa lilikuwa katika tishio la kukosa mafuta kabisa kutokana na ukosefu wa bidhaa hiyo muhimu kwa uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

"Kuna siku moja usiku Sokoine aliniita usiku akaniambia kuwa kuna taarifa kwamba nchi ina mafuta ya kutosheleza kwa siku moja tu. Aliniamuru niitishe kikao usiku huo huo ili kuona ni namna gani tunanusuru nchi dhidi ya tatizo hilo. Pia alisema kama kuna meli ina mafuta iruhusiwe kupakua ili kuiepusha nchi na tatizo hilo," anasema.

Tatizo hilo pia anasema lilitokea alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, alipoteuliwa muda mfupi baada ya kifo cha Sokoine.

Anasema hali ya upatikanaji wa mafuta mkoani humo ilikuwa ngumu kwa kuwa yalikuwa yakipatikana kwa shida na pia yalitolewa kwa mgawo na mtu aliamuriwa apate kiasi gani.

Kutokana na hali hiyo, anasema alianzisha utaratibu kwamba kiingiacho si haramu bali kitokacho. Anasema ili kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikana na wananchi hawapati adha, aliagiza kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kuhakikisha kiasi kidogo cha mafuta kilichoko ndani kisitoke nje lakini kile kinachoingia kiruhusiwe.

"Jambo hili lilisababisha kuwapo kwa mafuta ndani ya mkoa bila tatizo kulinganisha na maeneo mengine. Kilimanjaro iliitwa OPEC (Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani)," anasema.

**UONGOZI WA MSUYA**

Cleopa Msuya alikuwa Waziri Mkuu kuanzia mwaka 1980 hadi 1983 na kuteuliwa tena katika nafasi hiyo mwaka 1994 hadi 1995 kama Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Katika kipindi cha kwanza, Kimiti alimsaidia Msuya akiwa Waziri wa Nchi anayeshughulikia serikali za mitaa na vyama vya ushirika.

Anasema alimsaidia Msuya katika utaratibu wa kutunga sheria mbalimbali. Miongoni mwa sheria hizo ni za kurekesha vyama vya ushirika na serikali za mitaa pamoja na uteuzi wa viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa na vyama vya ushirika.

Taasisi hizo zilivunjwa kutokana na sababu mbalimbali lakini ilionekana kuna haja ya kurejeshwa. Kwa mujibu wa Kimiti, katika kipindi hicho alipata uzoefu mkubwa namna sheria zinavyoandaliwa.

"Tulifanikisha kutungwa kwa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Mjini na Halmashauri za Wilaya). Tulipitisha pia Sheria ya Vyama vya Ushirika na kupitia kazi hiyo tukawa wazoefu katika masuala ya kutunga sheria. Tulikuwa na wataalamu ambao walitusaidia na kwa kiasi kikubwa walitujengea uwezo katika kujua majukumu yetu katika sheria," anasema.

Kuhusu Msuya, Kimiti anamwelezea kuwa alikuwa msimamizi wa mambo na mtu wa kufuatilia utekelezaji wa majukumu. Pia anasema alikuwa anapenda sheria, kanuni na taratibu zifuatwe.

Katiba mabadiliko ya Baraza la Mawaziri mwaka 1983, Msuya aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na nafasi yake kuchukuliwa na Sokoine. Kimiti anasema anadhani alipelekwa kwenye nafasi hiyo (Wizara ya Fedha) ili kuweka nidhamu katika kuzitafuta na kuzitumia.

**TATHMINI YA MARAIS**

Kimiti katika maisha yake amefanya kazi na marais watatu-Nyerere, Ali Hassan Mwingi na Benjamin Mkapa katika nafasa tofauti za uwaziri na ukuu wa mkoa. Amawaelezea viongozi hao kuwa kila mmoja alikuwa na misinjgi yake katika uongozi wa nchi. Hata hivyo anesema wote walikuwa makini katika staili ya uongozi wao kutokana na nyakati na mazingira ya kinchi katika mambo mbalimbali.

Anasema chini ya Nyerere ambaye alitawala nchi kwa takriban miaka 24, alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na baadaye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Anamwelezea Nyerere kuwa alichukua uongozi wa nchi kutoka kwa wakoloni hivyo kazi yake kuwa ilikuwa kuhakikisha Watanzania wanajitawala.

Chini ya uongozi wake, anasema kuna mipango mingi ambayo iliandaliwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi ikiwamo ujenzi wa uchumi na huduma mbalimbali za kijamii kama vile afya na elimu.

"Ndiyo maana wakati wa uongozi wa Nyerere, kulikuwa na mambo mengi yalianzishwa kama Azimio la Arusha, Siasa ni Kilimo na Mipango ya Maendeleo ya Viwanda. Yote hiyo ni kwa ajili ya kuijenga nchi. Lakini kwa ujumla, Nyerere alijenga taifa na maadili," anasisitiza.

Kuhusu Mwinyi, ambaye wakati wa uongozi wake alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kagera na baadaye Mbeya, anasema aliongoza taifa kwa kufuata misingi ya Nyerere katika kusimamia nchi kusimama kiuchumi.

Anasema katika uongozi wake, Mwinyi alifungua milango ya uchumi na kusimamia mageuzi mbalimbali ya kiuchumi.

Wakati wa ngwe ya kwanza ya uongozi wa Mkapa, mwanasiasa huyo alikuwa Waziri wa Kilimo na baadaye Kazi na Maendeleo ya Vijana. Anamwelezea Mkapa kuwa alikuwa kiongozi aliyekuwa na dhamira kujenga uchumi na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

"Katika kutimiza hayo, Mkapa alisimamia ubinafsishaji wa mashirika na kuongeza mapato kupitia kodi pamoja na kuziba mianya ya rushwa na upotevu wa mapato. Katika kipindi chake ukusanyaji wa mapato uliongezeka, hivyo nchi kuwa na uwezo wa kuendesha miradi ya maendeleo kutokana na uwapo wa mapato," anasema.

*Kesho, sehemu ya nne na ya mwisho ya mwendelezo wa simulizi zake, itaangazia safari ya mito, milima na mabonde ya maisha yake.

Nipashe
Spotika



NYOTA WA5 WALIOFANYA VIBAYA BAADA YA KUTUA MAN UNITED UK. 12-13



FELIX



SON

# WACHEZAJI WATANO WALIORUDISHA KIWANGO CHAO MSIMU HUU

**LONDON,** England

KIWANGO ni kipengele muhimu kwa mchezaji wa soka. Umuhimu wake katika hatua za mwanzo za kampeni mpya hauwezi kupitwa. Kwa wanasoka, kugundua upya uchezaji wao mapema katika msimu kunaweza kuweka mwelekeo wa kampeni nzima.

Si tu kwamba huongeza kujiamini kwa mchezaji mmoja mmoja, lakini pia huishia kuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya timu. Wachezaji walio katika kiwango cha juu wana uwezekano mkubwa wa kufunga mabao, kutengeneza nafasi kwa wachezaji wenzao na kutoa michango muhimu uwanjani.

Kuwa na wachezaji walio katika kiwango kizuri huwezesha timu kuanza msimu kwa kasi, kupata kasi mapema na kujenga msingi thabiti wa malengo yao ya msimu.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao wamerudi tena katika kiwango chao msimu huu, haya sasa...

**#5 Takumi Minamino (AS Monaco)**

Baada ya kukaa kwa miaka miwili katika Klabu ya Liverpool, mshambuliajia wa Japan, Takumi Minamino angetarajia kuboresha maisha yake alipokamilisha uhamisho wa kwenda AS Monaco msimu wa majira ya joto wa 2022.

Lakini alivumilia kampeni ya kwanza iliyosahaulika nchini Ufaransa, akifunga mara moja tu na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 25 kwenye mashindano yote msimu wa 2022-23. Lakini akiwa na wakosoaji na wapinzani mgongoni mwake, amefufuka tena muhula huu.

Kuanza kwa msimu vibaya kumemfanya ya Minamino kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwezi wa Ligue 1 kwa Agosti. Minamino anaonekana kuwa hatimaye amepiga hatua yake hapo AS Monaco. Amefunga mabao matatu na kutoa asisti tatu katika mechi sita za Ligue 1 hadi sasa msimu huu.

**#4 Federico Chiesa (Juventus)**

Baada ya maonesho yake ya kuvutia kwenye Euro 2020, Chiesa alikosa mechi 73 za Juventus kwenye mashindano yote katika misimu miwili iliyopita kutokana na matatizo mengi ya majeraha. Lakini anaonekana kurejea polepole kwenye ubora wake kwa 'Bianconeri' katika hatua za mwanzo za kampeni mpya.

Chiesa alifanikiwa kufunga mabao manne pekee na kutoa pasi za mabao sita katika mechi 33 za mashindano yote akiwa na Juventus msimu uliopita. Winga huyo tayari ameshatikisa nyavu mara nne na kutoa asisti kwenye mechi sita za Serie A hadi sasa msimu huu wa 2023-24.

**#3 Yves Bissouma (Tottenham Hotspur)**

Yves Bissouma alivumilia msimu mgumu wa kwanza akiwa Tottenham Hotspur. Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anaonekana kurudi kwenye kiwango chake katika hatua za awali za msimu wa 2023-24. Tottenham imekuwa katika kiwango cha kuvutia chini ya kocha mpya, Ange Postecoglou na safu yao ya kiungo iliyojaa mafuta imekuwa muhimu kwa uchezaji wao.

Bissouma amefanya vema kwenye safu ya kiungo ya Tottenham hadi sasa msimu huu. Uchezaji mkali wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Mali na uwezo wake bora wa kusoma mchezo umeisaidia Spurs kuwakatisha tamaa wapinzani katikati mwa uwanja.

**#2 Joao Felix (Barcelona)**

Joao Felix aliwasili Barcelona kwa mkopo kutoka Atletico Madrid msimu huu wa majira ya joto. Baada ya kutofautiana na Diego Simeone, hakukuwa na shaka yoyote juu ya dhana kwamba mustakabali wa mshambuliaji huyo mchanga wa Ureno uko mbali na Atletico. Ikiwa kiwango chake cha msimu wa mapema kilikuwa cha kupita, Felix anaweza kuwa ametua kwenye klabu sahihi kwake.

Hakika amegeukia mtindo huo tangu ajiunge na Barcelona. Ujanja na ubunifu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, umeongeza makali kwenye mchezo wa klabu hiyo ya 'Katalunya' ndani ya tatu ya mwisho. Katika mechi sita kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu, Felix amefunga mabao matatu na kutoa asisti mbili.

**#1 Son Heung-min (Tottenham)**

Baada ya kushiriki kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England na Mohamed Salah msimu wa 2021-22, mashabiki walishangazwa kuona Son Heung-min akishuka kiwango msimu uliopita. Son alishindwa kufikia kiwango chake cha kawaida katika msimu wa 2022-23.

Lakini anaonekana kuwa na dhamira ya kubadilisha mambo katika muhula huu. Winga huyo mashuhuri wa Korea Kusini tayari amepata hat-trick yake ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu na anaonekana kuwa katika hali ya kuwa kwenye kiwango bora zaidi.

Amefaidika kwa kuwa na mbunifu James Maddison karibu na ametumia vizuri huduma ambayo amekuwa akipokea. Katika mechi saba kwenye michuano yote hadi sasa kwa upande wa kocha Postecoglou, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao matano.

**ISIKUPITE**

KLABU nne za ligi tano bora Ulaya ambazo hazijapoteza mechi yoyote tangu kuanza kwa msimu huu wa 2023/24; #4 Barcelona imeshinda sita, sare tatu kati ya tisa ilizocheza, #3 Arsenal (imeshinda sita, sare mbili kati ya nane ilizocheza), #2 Tottenham (imeshinda sita, sare mbili kati ya nane ilizocheza), #1 Bayer Leverkusen (imeshinda sita sare moja kati ya saba ilizocheza).



## Extra Time

# NYOTA WA5 WALIOFANYA VIBAYA BAADA YA KUTUA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

SI kila wakati rasilimali nyingi zinahakikisha mafanikio katika soka. Mapungufu ya Manchester United kwenye soko la uhamisho wa wachezaji katika muongo mmoja uliopita ni mfano tosha wa hili.

**'Mashetani Wekundu' hao hawajakabiliwa na tatizo la uhaba wa fedha na wameweza kuwavuta baadhi ya nyota wakubwa wa mchezo huo hadi pale Old Trafford.**

Hata hivyo, ni hatua chache tu kati ya hizi za kiwango cha juu ambazo zimefanikiwa kwa Manchester United. Wachezaji wengi wakubwa ambao wamecheza United wamepata mafanikio katika klabu nyingine kabla au baada ya muda wao hapo United.

Makala haya inawatazama wachezaji mastaa watano waliofanya vibaya baada ya uhamisho wao wa kutua Man United, twende sasa...

### #5 Donny van de Beek

Uhamisho wa Donny van de Beek kwenda Manchester United bila shaka umekuwa wa kukatisha tamaa kwa pande zote zinazohusika. Tangu kuwasili kwake Old Trafford mwaka wa 2020, kiungo huyo wa kati wa Uholanzi amekuwa na wakati mgumu kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza.

Licha ya kuonesha uwezo na kipaji wakati alipokuwa Ajax, amezidiwa kwa kiasi kikubwa na safu nyingine za kiungo hapo United. Majeraha na muda usiobadilika wa kucheza umeathiri uwezo wake wa kuzoea Ligi Kuu England na kuleta athari kubwa kwenye mwenendo wa timu.

Ukosefu huu wa muda wa kucheza na nafasi ya kuonesha uwezo wake umewachanganya mashabiki na mchezaji mwenyewe, na ni wazi kwamba uhamisho wake wa kwenda Man United haujafanikiwa kama ilivyotarajiwa.

Katika mechi 62 kwenye michuano yote akiwa na Mashetani Wekundu, Mholanzi huyo amefunga mabao mawili pekee na kutoa asisti mbili.


### #4 Paul Pogba

Muda wa Paul Pogba katika Klabu ya Manchester United umekuwa na wakati mzuri, lakini hatimaye ukaonekana kuwa mbaya kwa sababu nyingi. Licha ya kutoa mwanga wa mara kwa mara wa kipaji chake kikubwa na uwezo wa kushawishi michezo, lakini mambo yalikuwa tofauti.

Kiwango cha Mfaransa huyo kilikuwa kikitofautiana na vipindi vya uchezaji wa kipekee vikifuatiwa na vipindi virefu vya hali ya wastani.

Zaidi ya hayo, uhusiano wake na klabu hiyo na mashabiki wake ulikuwa na tetesi za uhamisho na wakala wake ambaye alikuwa akizungumza waziwazi, marehemu Mino Raiola, akitoa taarifa hadharani kuhusu nia yake ya kuondoka.

Mambo haya yote yalichangia hisia ya uwezo usiotimizwa. Hii imewafanya wengi kuamini kuwa muda wa Pogba katika Klabu ya Manchester United ulipungua kwa matarajio makubwa yaliyoambatana na kurejea kwake klabuni hapo.



SANCHO

### #3 Jadon Sancho

Inaonekana muda wa Jadon Sancho ndani ya Manchester United unaweza kumalizika hivi karibuni. Winga huyo wa England alijiunga na United huku kukiwa na mvuto mkubwa katika majira ya joto ya 2021. Lakini akiwa Old Trafford, amekuwa kivuli cha mchezaji ambaye alikuwa na wakati wa kuvutia kule Borussia Dortmund.

Sancho ameshindwa kubadilika katika safu ya uchezaji thabiti katika muda wake wote klabuni. Mzozo wa hivi majuzi kati yake na Kocha wa United, Erik ten Hag, umemfanya Sancho kutokuwa na uhakika wa kuendelea kuichezea klabu hiyo.

Kocha huyo wa Uholanzi alimkosoa Sancho katika mkutano na waandishi wa habari ambapo kijana huyo alijibu kupitia kwenye mitandao ya kijamii. Haionekani kama Mwingereza huyo anataka kurejea kwenye kikosi hicho kwani ripoti zinadai kuwa amekataa kumwomba msamaha Ten Hag kwa kitendo chake hicho.

Anguko la Sancho linaweza kuoneshwa vema zaidi kwa kutumia takwimu zake. Akiwa Dortmund, alifunga mabao 50 na kutoa asisti 64 katika mechi 137 katika mashindano yote. Akiwa United, amefunga mabao 12 pekee na kutoa pasi za mabao sita kwenye mechi 82 katika michuano yote.

### #2 Angel Di Maria

Muda wa mwaka mmoja wa Angel Di Maria katika Klabu ya Manchester United ulikuja wakati wa kusahaulika kwenye historia ya klabu hiyo. Winga huyo wa Argentina aliwasili Old Trafford kwa uhamisho wa hali ya juu kutoka Real Madrid, huku matarajio makubwa yakiwekwa kwenye mabega yake.

Hata hivyo, muda wake nchini England ulitawaliwa na kutofautiana na mapambano ya majeraha. Ingawa alionesha picha za kipaji chake isiyoweza kukanushwa na nyakati za kushangaza, alijitahidi kuzoea umbo la Ligi Kuu.

Nje ya uwanja, alikumbana na masuala binafsi, ikiwa ni pamoja na kuibiwa nyumbani kwake, ambayo iliathiri zaidi kiwango chake. Hatimaye, uchezaji duni wa Di Maria na kuripotiwa kutofautiana kati yake na kocha wa wakati huo, Louis van Gaal, kulisababisha kuondoka kwake kwenda Paris Saint-Germain baada ya msimu mmoja pekee.

Hili liliwaacha mashabiki wa Manchester United wakiwa wamekata tamaa kwani walikuwa na matumaini kwamba Di Maria ndiye angekuwa mchezaji ambaye angewasaidia kurejea kileleni mwa soka la Uingereza. Alifunga mabao manne pekee na kutoa asisti 12 katika mechi 32 kwenye mashindano yote akiwa na Mashetani Wekundu hao.

### #1 Alexis Sanchez

Video ya Alexis Sanchez ya tangazo la uhamisho ambapo alikuwa akicheza "Glory, Glory, Man United" kwenye piano labda ilikuwa wakati wake bora zaidi akiwa na jezi ya United.


Kulikuwa na msisimko mkubwa wakati raia huyo wa Chile akiwasili klabuni hapo, hali ambayo alishindwa kuizalisha kutokana na uchezaji wake uwanjani hapo baadaye. Mambo yote yakizingatiwa, itakuwa ni ukatili kumlaumu Sanchez peke yake kwa muda wake United kwenda mrama.

Alikuwa hafai kwa Manchester United ya Jose Mourinho na alionekana hajui lolote uwanjani. Kuchanganyikiwa kuliendelea kuongezeka kwa kila utendaji duni na haukupita muda mrefu kabla ya kupelekwa kwa mkopo kwenda Inter Milan na mwishowe akajiunga nao kwa uhamisho wa kudumu mwaka 2020.

Sanchez alifunga mabao matano pekee na kutoa pasi tisa za mabao katika mechi 45 kwenye mashindano yote akiwa na Manchester United. Hii ilikuja kutokana na kiwango cha kuvutia cha mshambuliaji huyo akiwa pale Arsenal, ambapo alifunga mabao 80 na kutoa pasi za mabao 45 katika mechi 166 alizocheza kwenye michuano yote.

## Nukuu

"Nilipochagua kuhama kutoka City kwenda Arsenal, Edu na Arteta [Mikel], walizungumza nami na niliweka wazi kuwa ningependa kucheza kama 'tisa'. Hili lilikuwa wazo la Arsenal - kwangu kucheza kama 'tisa', huru. Msimu huu umekuwa tofauti. Tumekuwa na majeraha na katika mechi tatu zilizopita, nilicheza winga. Kwa muda, nilifikiria kusema kwamba nataka kucheza kama 'tisa'. Lakini niko hapa kusaidia timu. Nimebarikiwa na Mungu kuwa na kipaji hiki na uwezo wa kucheza katika nafasi tatu za mbele. Napendelea kutochagua," **mshambuliaji wa Arsenal, Mbrazili Gabriel Jesus**



"Cristiano Ronaldo ni mzuri, lakini Messi [Lionel] ni bora mara kumi yake. Messi anaweza kuwapita wapinzani wake katika mita ndogo ya mraba, wakati Ronaldo anahitaji nafasi zaidi," **mshambuliaji wa zamani wa Real Madrid, Klaas-Jan Huntelaar.**



"Sio jinsi tulivyotaka kwenda kwenye mapumziko ya kimataifa, lakini tutarejea pamoja, kama kawaida," **mshambulizi wa Norway, Erling Haaland, akizungumza kuhusu kupoteza mfululizo kwa Manchester City hivi karibuni kwenye Ligi Kuu England baada ya kuchapwa na Arsenal bao 1-0 kipigo hicho kikija ikitoka kupigwa mabao 2-1 na Wolverhampton.**





Mshindi wa mbio za Tigo Zantel International Marathon akipokea zawadi msimu uliopita.

# ZANZIBAR MARATHON KUIBUA VIPAJI, KUKUZA UCHUMI

**Na Mwandishi Wetu**

RIADHA ni mchezo ambao unakua kila kukicha na kuwapa vijana ajira zinazowawezesha kumudu na kuendesha maisha yao ya kila siku. Lakini mbali na ajira kushiriki kwenye riadha kunasaidia sana kujikinga na maradhi nyemelezi kutokana na wakimbiaji kufanya mazoezi mara kwa mara.

**Tanzania imebahatika kuwa na vijana wengi ambao wanashiriki kwenye mchezo huu mkubwa duniani baada ya soka. Nchi hii ni kati ya zenye wanariadha wengi ambao kila mwaka wanapata fursa za kwenda kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa na kujiingizia kipato kwa kiasi kikubwa.**

Mfano wa wanariadha hao ni Alphonce Simbu ambaye kwa miaka ya karibuni amekuwa akiipeperusha vema bendera ya Tanzania na kuitangaza nchi kimataifa. Riadha pia imekuwa ikiitangaza nchi kimataifa kwa rasiliamali zake.

Katika visiwa vya Zanzibar kumekuwa na mashindano mbalimbali ya riadha ambayo hukusanya wanariadha kutoka visiwani humo na Tanzania Bara kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vya wakimbiaji.

Oktoba 29, mwaka huu, kunatarajiwa kufanyika mbio za marathon ziizoandaliwa na kudhaminiwa na kampuni ya simu ya Tigo Zantel na kupewa jina la 'Zanzibar International Marathon'.

Mbio hizi zinatarajiwa kukusanya maelfu ya wakimbiaji kutoka ndani na nje ya nchi. Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika kwa mara nyingine na kuwapa nafasi wanariadha watakaoshiriki kushinda zawadi mbalimbali.

Mbio hizi za Zanzibar Marathon, zinatagemewa kuongeza hamasa kwa wanamichezo visiwani humo pamoja na Tanzania Bara katika kuendeleza mchezo wa riadha.

Haya yanathibitishwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tigo Zantel upande wa Zanzibar ambao ndio waandaaji wa mashindano hayo, Azizi Saidi Ali, ambaye anasema mashindano hayo ni mahususi kwa ajili ya kukuza vipaji na kuendeleza mchezo wa riadha Zanzibar.

"Tunategeme wanariadha wengi kutoka Zanzibar, Tanzania Bara na nchi jirani kushiriki, haya ni mashindano makubwa yenye lengo la kukuza mchezo huu lakini pia kuitangaza Zanzibar Kimataifa," alisema Saidi.

Said anasema kauli mbiu ya mbio hizo kwa mwaka huu ni 'Tukutane kwenye Kibasi cha Zenji' kwa Spidi ya 5G, kwenye visiwa vya Karafuu kwa ajili ya Tigo Zantel Zanzibar International Marathon'.

Anasema malengo ya mbio hizo ni kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii kwa kuwekeza kwenye miradi na matukio yanayogusa hisia na maisha ya wananchi kupitia mbio hizo.

"Hii ni fursa kwa Watanzania, tunawaomba wajitokeze kwa wingi kujiandikisha kushiriki ili kufikia malengo," alisema Said.

Alisema kutokana na umuhimu na ubora wa mashindano hayo, usajili wake utafanyika kwa kidigitali, hivyo kila mmoja anaweza kujisajili mwenyewe kwa muda mfupi.

"Hii ni mara nyingine mbio hizi zinafanyia Zanzibar, utofauti ni kwamba mwaka huu, washiriki watatakiwa kuomba na kujisajili kwa njia ya mtandao.

"Maandalizi yanakwenda vizuri, tunawaomba wadau mbalimbali kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa njia ya kidijitali na kushiriki mbio hizi," anasema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau wa riadha, wamesema mbio za mwaka huu za Tigo Zantel Zanzibar International Marathon zitasaidia kukuza sekta ya utalii wa michezo ambayo imeonesha kukua kwa kasi duniani sambamba na kuitangaza Zanzibar kimataifa.

Mmoja wa wadau hao, Rashid Mohamed Rashid, amesema, sekta ya utalii kwa Zanzibar ina uwanja mpana hasa ukizingatia kuwa eneo hilo ni la uchumi wa bluu ambao ndiyo mkakati wa serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Aidha, mdau mwingine na shabiki wa mchezo wa riadha, Omar Amir Suleiman, anasema ni vema waandaaji wa mashindano hayo kuedelea kuyatangaza na kuwahamasisha wananchi wa Zanzibar kushiriki.

"Michezo hujenga afya kutokana na wananchi wa Zanzibar kuhamasika kwa kiasi kikubwa kushiriki mbio mbalimbali kila zinapotokea, hii itasaidia kuwa na wananchi wenye afya bora na wakakamavu," alisema na kuongeza,

"Nashauri pia waandaaji waangalie namna ya kuleta pia mbio za wazee na watoto ili kushirikisha watu wa rika zote na kuwajengea afya imara," alisema.

## JE, WAJUA?



TANGU atue Old Trafford mwaka 2020, kiungo Donny van de Beek, ameitumikia Manchester United katika mechi 62 kwenye michuano yote huku akifunga mabao mawili pekee na kutoa asisti mbili.



# Hatima madaktari tarajali bado giza

## -Waiangukia serikali, miezi 10 wako nyumbani

**Na Jenifer Gilla**

MADAKTARI tarajali 366 walifeli mtihani wa Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT), hawajui hatima yao kutokana na ukimya wa kamati iliyoundwa kuchunguza kufeli kwao.

Wamesema hali hiyo inawaathiri kitaaluma kwa kuwa baadhi yao wana miezi 10 sasa tangu wamalize mafunzo. Wako nyumbani, hawafanyi kazi yoyote inayohusu taaluma yao ilhali wanahitaji kujifunza kwa vitendo.

Machi 22 mwaka huu, madakatri 640 walifanya mtihani huo. Kati yao 270 sawa na asilimia 43 walifaulu huku 366 (asilimia 57) wakifeli. Kwa mujibu wa MCT, wanafunzi hao wamefeli mtihani huo kutokana na uwezo mdogo.

Lakini, Juni 21 mwaka huu, madaktari hao walimwandikia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan barua ya wazi yenye hoja kadhaa zinazohusu malalamiko hayo na nakala yake kupelekwa Wizara ya Afya.

Baada ya kupokea nakala hiyo, Waziri wa Afya, Waziri Ummy aliunda kamati yenye wajumbe 13 ikiongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali mstaafu, Prof. Muhamad Bakari. Ilipewa mwezi mmoja kuchunguza msingi wa malalamiko yaliyotolewa na madaktari tarajali hao.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa jana na mwakilishi wa madaktari hao, Amani Mwakalobo, ilibainisha kuwa tangu kamati hiyo ipewe jukumu la kuchunguza suala hilo, imepita miezi miwili sasa na wizara haijasema chochote. Ni jambo linalowapa hofu kwamba huenda wasipate haki yao.

Vilevile, Mwakalobo alisema katika taaria yao hiyo kwamba wameshangazwa na kitendo cha kutokuwa na mwakilishi wao yeyote katika kamati ya Waziri Ummy ilhali wao ndiyo walalamikaji.

Hali hiyo, Mwakalobo alisema inawapa wasiwasi kama madai yao yatafanyiwa kazi inavyostahili.

Alibainisha kuwa mnamo Septemba 19 mwaka huu, kamati hiyo iliwaita madaktari tarajali hao na kuwahoji. Sasa mwezi umepita bila kutolewa ripoti yoyote ilhali kamati hiyo ilipewa mwezi mmoja kufanya uchunguzi.

“Mpaka sasa ni miezi miwili, bado wizara haijasema hatima ya madaktari tarajali hawa licha ya kamati kuelekezwa kufanya kazi ndani ya mwezi mmoja kuchunguza malalamiko yao,” alisema Mwakalobo katika taarifa yao hiyo.

Aliiomba wizara iwasaidie vijana hao kwa kuwapatia leseni ili waendelee kazi, wasaidie familia zao zilizotumia gharama kubwa kuwasomesha kwa miaka mitano na kupitia mwaka mmoja wa utarajali.

Mwakalobo alisema vijana hao walifanya kazi chini ya madaktari bingwa na madaktari bingwa bobezi na kuona wamekuwa vizuri kuendelea kutibu wananchi.

Alisema inasikitisha kuona wameshindwa kupatiwa vyeti vya kumaliza mafunzo hayo kutokana na mtihani wa machaguo wa siku moja unaotolewa na MCT. Hata hivyo, baraza hilo na mtihani wake ni kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mnamo Agosti 14 mwaka huu, Waziri Ummy aliunda kamati iliyoiita huru yenye wajumbe 13 kuchunguza malalamiko ya madaktari waliohitimu mafunzo ya utarajali juu ya mitihani inayotolewa na MCT kabla na baada ya usajili.

Kamati hiyo chini ya Prof. Bakari itakiwa kufanya kazi kwa mwezi mmoja kwa kufuata hadidu za rejea zilizoainishwa na wizara ili kuchunguza msingi wa malalamiko yaliyotolewa na madaktari tarajali hao.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jaffar Shekimweri, akikabidhi mayai kwa viongozi wa Kampuni ya SAB Investments ambao waliratibu Kampuni ya Changia Yai kwa Watoto wenye Uhitaji kama sehemu ya kuhamasisha jamii kujitoa kwa wenye uhitaji wakati wa maadhimisho ya Siku ya Yai Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaanika mikakati uboreshaji huduma za afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, amesema serikali imejipanga kuweka nguvu katika kuboresha ubora wa huduma za afya, kuahidi kuendeleza mafanikio ya mradi wa HPSS Tuimarishe Afya.

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati akifunga kikao cha siku mbili cha kuhitimisha mradi huyo uliokuwa ukitekelezwa kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Afya kwa ufadhili wa Serikali ya Uswisi.

Maeneo ambayo mradi umefanya kazi ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) mshitiri pamoja na uimarishaji wa utengenezaji wa vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema serikali imefanya kazi ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa na rufani na kwa sasa nguvu kubwa inaelekezwa katika kuboresha huduma kwa kuwa bado kuna pengo kwenye eneo hilo.

Alisema ni muhimu kuangalia namna ya matengenezo ya vifaa tiba kwa kuwa ni mara nyingi vifaa vimekuwa vikiharibika kitu kidogo na kupelekwa stoo.

“Tunatumia fedha nyingi sana kununua vifaa tiba mara kwa mara vinatumika kwa muda mfupi na kushindwa kufanya marekebisho madogo, mradi wa HPSS Tuimarishe Afya umetuwezesha namna ya kuweka mifumo imara ya matengenezo ya mara kwa mara ya vifaa tiba na miundombinu mingine ili kutoa huduma vizuri,” alisema.

Mwenyekiti wa Makatibu Tawala wa Mikoa, Rehema Madenge, alisema mradi huo umeleta utaratibu wa mshitiri umesaidia upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za dawa pale ambapo hazipatikani kutoka MSD kwa wakati.

# Watoto wenye VVU kutambuliwa, kupewa huduma bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC) imekuja na mradi wa ‘USAID Tuwajali watoto’ kwa ajili ya watoto wanaoishi na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) ili kuwatambua, kuwaanzishia dawa na kupata huduma bora za afya.

Mradi huo umefadhiliwa na Mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Maambukizo ya VVU (PERFAR) kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo la Kimataifa (USAID).

Mkurugenzi Mtendaji wa CSSC, Peter Maduki alisema: “Tunafanya kazi katika mikoa 11 nchini na kwa kipekee na tunafanya kazi na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya kama kituo cha mfano ambacho kitakuwa na wataalamu waliofundishwa na watakaotumika kwenda kuwafundisha wataalamu wengine”.

Alibainisha kuwa mradi huo utagharimu Dola za Marekani milioni 13.6 na zitatumika kuboresha huduma kwenye mikoa na kituo hicho na utatekelezwa kwa miaka mitano hadi mwaka 2028.

Mkurugenzi wa mradi huo, ambaye ni Daktari Bingwa wa Watoto, Dk. Theopista Masenge alisema mradi huo utatekelezwa na CSSC na washirika wenza ambao ni CRS na Afya Plus.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwafuatilia wajawazito wanaishi na VVU, watoto waliozaliwa na VVU, watoto waliopata au kuishi na maambukizi wenye umri wa miaka 0- 19.

Aidha, alisema kutakuwa na kampeni ya nyumba kwa nyumba kuhakikisha jamii imeelewa na kuwashirikisha viongozi wa dini ili kila mzazi lazima ajue hali ya afya ya mtoto.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya kutoka CSSC, Dk. Josephine Balati alisema hadi sasa watoto 90,000 hadi 110,000 wanaishi na VVU, huku asilimia 60 ya watoto hao wamepimwa na kujua hali zao.

# RC akemea imani potofu kuhusu ulaji mayai

**Na Mwandishi Wet,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema jamii inapaswa kupewa elimu kuhusu ulaji wa mayai ili kuondoa imani potofu ikiwamo mama mjamzito kuzaa mtoto kwenye kipara anapokula mayai.

Aliyasema hayo mkoani hapa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Yai Duniani, iliyofanyika katika Viwanja vya Mashujaa vya zamani, kuhudhuriwa na mamia ya wananchi.

Senyamule alisema Siku ya Yai Duniani inaweza kutumika vyema katika jamii kuleta hamasa na elimu kwa kuondoka pia imani potofu juu ya ulaji wa mayai.

Alisema kuna baadhi ya watu wanawakataza wajawazito kula mayai wakidai kuwa watazaa watoto wenye vipara.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Jaffar Shekimweri, alisema ulaji wa mayai unafaida nyingi mwilini huku akiipongeza Kampuni ya SAB Investment kwa kuhamasisha jamii kula na uchangiaji wa mayai kwa watoto wenye uhitaji.

Mkurugenzi wa SAB Investment, Saida Bwanakheri, alisema kupitia kampeni hiyo wameweza kuvifikia vituo vitatu vya mkoani Dodoma.

Alivitaja vituo hivyo ni kituo cha kulea watoto yatima cha Al Rahmaan, Binti Shams, Chang’ombe Kariba, Shule ya Sekondari Chinangali.

## Msongamano wanafunzi kwenye mabweni wamgusa mbunge

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza ameahidi kuchangia Sh. milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa bweni jipya katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Gari Jembe ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye mabweni.

Alitoa ahadi hiyo kwenye mahafali ya kwanza ya kidato cha nne shuleni hapo ambapo alisema wanafunzi wamekuwa wakiongezeka kila mwaka hali ambayo imeanza kusababisha upungufu wa miundombinu hiyo.

Alisema shule hiyo imekuwa ikipokea wanafunzi kutoka katika kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwamba ndiyo shule ya mfano kwa Mkoa wa Mbeya.

"Nimeambiwa kwamba kwa mwaka huu pekee watoto wa kidato cha kwanza wapo zaidi ya 100, sasa tunatakiwa tuanze kujihami, mimi kutoa kwenye mfuko wangu Sh. milioni 10 na tutaendelea kushirikiana kwenye shughuli zingine," alisema Njeza.

Vilevile aliahidi kununua runinga ya kisasa kwa ajili ya shule hiyo ili kuwasaidia wanafunzi kufuatilia matukio mbalimbali yanayoendelea duniani kupitia taarifa za habari na matukio mbalimbali.

Katika hatua nyingine aliwapongeza walimu wa shule hiyo kwa ubunifu wao katika kukabiliana na upungufu wa miundombinu hasa kwa kubadili baadhi ya vyumba vya madarasa ambavyo vilikuwa havitumiki na kuvifanya kuwa maabara za baadhi ya masomo ya sayansi.

# Ajali za barabarani zaua watu 133 kila mwezi nchini

**Na Christina Mwakangale**

WATU 1,198 wamepoteza maisha kwenye ajali 1,334 zilizotokea katika kipindi cha miezi tisa iliyopita, ikiwa ni ongezeko la ajali 30 (asilimia 2.5) kulinganishwa na kipindi kama hicho mwaka jana.

Hiyo ina maana kwamba, kuna wastani wa vifo vya watu 133 kwa mwezi au vinne kila siku kutokana na ajali nchini.

Takwimu hizo zilizotolewa na Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, zimeainisha kundi la vyombo vya moto ambavyo vimesababisha vifo zaidi ni pamoja na usafiri wa bodaboda, ajali zake 339 zikisababisha vifo kwa watu 263.

Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani Tanzania, Kamishna Msaidizi Michael Deleli alibainisha takwimu hizo mwishoni mwa wiki wakati wa Kongamano la Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA), akimwakilisha Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini.

Alisema kikosi hicho kimekuwa kinakumbana na changamoto kadhaa katika kudhibiti ajali barabarani kama vile kutokuwapo kamera za barabarani na askari wachache wa usalama barabarani kutokana na ongezeko kubwa la vyombo vya moto, hasa bodaboda zinazokadiriwa kuwa zaidi ya milioni mbili.

"Kuna bodaboda zaidi ya milioni mbili nchini, lakini askari wa usimamizi wa bodaboda hizo ni walewale ambao zamani ilikuwa ni kusimamia madereva wa magari na watembea kwa miguu, hivyo idadi yao ni ndogo. Kwahiyo, wadau wa kisimamia usalama barabarani wanapoongezeka tunaona ni msaada mkubwa kwetu.

"Ajali kwa mwaka huu kipindi cha miezi tisa zimesababisha vifo 1,198 ikiwa ni ongezeko la vifo 35 sawa na asilimia 2.8 kulinganisha kipindi kama hicho mwaka jana. Mwaka huu kwa miezi tisa, majeruhi wa ajali ni 1,833, kuna ongezeko la majeruhi 98 kulinganishwa na mwaka jana, sawa na asilimia 5.6," alisema Kamishna Deleli.

Aliongeza kwamba umefika wakati wa kuwabadili fikra watumiaji wa vyombo vya moto kuwa watii wa sheria za usalama barabarani bila shuruti, akisema miongoni mwa vitu vinavyogharimu familia nchini ni ajali. "Katika mtaa huwezi ukamaliza mwezi bila kusikia tukio la ajali. Tunatamani kila mmoja awe na utii wa sheria, ila bado changamoto ni kubwa kwa sababu elimu ya usalama barabarani mtu anaanza kuwa nayo anapoanza kumiliki chombo. Kimsingi elimu hii inatakiwa ianze ngazi ya familia tangu kwa watoto wa shule ya msingi.

"Miaka ya 1990 vifo vilikuwa takribani 3,000 au 4,000 ila ukweli ni kwamba hatutamani kuona ajali hizo. Kuna ongezeko la vyombo vya moto nchini kuliko miaka hiyo. Miaka hiyo nchi ilikuwa watu kama milioni 40 sasa milioni 60, ukifanya uwiano tumepunguza vifo, ajali na majeruhi kwa asilimia 50," alifafanua.

Alisema jeshi limeendelea kutoa elimu. Wamezifikia shule 3,302 na wanafunzi 1,425,389.

Mwenyekiti wa RSA Taifa, DCP Mohamed Mpinga, alisema asasi hiyo imelenga kutoa elimu ya usalama barabarani kwa jamii, huku akiishukuru kampuni ya Dangote kufanikisha kongamano hilo ambalo ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Usalama Barabarani, iliyofanyika mkoani Mtwara.

Alisema RSA kwa kushirikiana na kampuni hiyo chini ya uratibu wa Kamati ya Usalama Barabarani mkoani huhumu kuanzia Oktoba 2 mwaka huu, wametoa mafunzo kwa shule za msingi 10, madereva wa Dangote, kuelimisha wakazi wa vijiji hasa vya kando ya barabara.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Ngonga iliyoko wilayani Kyela wakichota maji kwenye moja ya bomba la kupampu wilayani hapo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Viongozi waliofariki dunia kwenye ajali wafikia saba

**Na Eizabeth John,** MAKETE

IDADI ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata za Ipepo, Tandala, Lupila na Lupalilo wilayani Makete mkoani Njombe waliofariki dunia kwa ajali ya gari, imefikia saba baada ya mmoja kukumbwa na umauti wakati akiendelea na matibabu.

Aliyefariki dunia jana ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Kata ya Lupalilo, Blasia Sanga aliyekuwa amelazwa katika Hospitali ya Mission ya Consolata Ikonda, wilayani Makete.

Waliofariki dunia Oktoba 13 mwaka huu ni Tumaini Mbilinyi - Katibu wa CCM Kata ya Tandala, Heblon Mbilinyi - Katibu Mwenezi CCM Kata ya Tandala, Eva Sanga - Katibu UWT Kata ya Lupila, Linus Sanga - Mwenyekiti wa Wazazi CCM Kata ya Tandala, Spelancia Sanga - Katibu wa UWT Kata ya Ipepo na Luth Sanga - Mwenyekiti UWT Kata ya Lupila.

Jana mamia ya wananchi, viongozi wa CCM na serikali walishiriki katika ibada ya kuaga miili sita ya viongozi hao.

Akitoa salamu za rambirambi, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Halima Mamuya ambaye ni mlezi wa mkoa wa Njombe, alisema ni muhimu msiba huo mzito usiwagawe bali uwaimarishe kwa kuwa kila mmoja ataondoka duniani kwa kadri alivyopangiwa na Mungu.

"Niliwakuta mkiwa wamoja, endeleeni kuwa wamoja na sisi wote tutashirikiana na ninyi katika msiba huu na katika mambo yote mengine ya kuleta maendeleo katika wilaya hii ya Makete, mkoa huu wa Njombe na Tanzania yetu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alitoa pole kwa familia. Serikali itaendelea kuhakikisha familia zinawezeshwa kwenye msiba pamoja na matibabu kwa majeruhi wa ajali hiyo.

"Tumekimbiliwa na tumeliliwa na kila mtu mmeona salamu za Rais Samia Suluhu Hassani ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa.

"Tulipokuja hapa juzi kwenye Hospitali ya Ikonda maelekezo ya Rais kwenye jambo hili ni kwamba serikali ichukue dhamana ya kuhakikisha marehemu wote wanahifadhiwa kwa heshima zote kama Watanzania, miili kufikishwa sehemu sahihi kwa kusafirishwa na shughuli zote zinazohusu msiba zinafanywa na serikali. "Kwa maelezo ya daktari wa mkoa katika wale majeruhi mmoja atapaswa kupelekwa MOI Dar es Salaam na tutahakikisha hilo linafanyika. Niwahakikishie watu wa Makete na familia hizi zote hatuwezi kurudisha uhai wa ndugu zetu, lakini tunaomba mpokee faraja hii kubwa ya serikali hususani faraja kubwa ya Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili," alisema.

Katibu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) , Robert Kitundu, aliwasilisha salamu za rambirambi za kanisa hilo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Makete, Clement Ngajilo, aliwaomba wana-Makete licha ya kupitia kipindi kigumu, wasigawanyike badala yake wamwombe Mungu.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa, Venance Mabeyo, aliwataka wananchi wa Makete kujipa matumaini na kumwomba Mungu kuwapa nguvu ya kustamili tukio hilo kubwa ambalo hawakulitarajia.

Akizungumza kwa niaba ya familia zilizofikwa na msiba huo, Ayubu Lwila aliishukuru serikali kwa kugharamia shughuli zote za mazishi.





# Umaskini wa kipato watajwa chanzo migogoro ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHEHA wa Paje Mkoa wa Kusini Unguja, Muhammed Rajab Makame, amesema umaskini wa kipato kwa wananchi umechukua nafasi kubwa na kusababisha mivutano ya migogoro ya ardhi.

Alisema licha ya uwepo wa umaskini wa kipato lakini wananchi kutokuwa na ufahamu wa utafsiri wa sheria katika ununuzi wa ardhi nao ni miongoni mwa sababu ya migogoro hiyo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia mvutano uliopo kijijini hapo wa umiliki wa ardhi kwa wawekezaji Paulina Czachowsia wa Kampuni Feel Good Enterprises na mmiliki wa Hoteli ya Roland Aluna wanaovutana kuhusu eneo la ardhi ambapo hoteli hizo zimepakana.

Alisema jambo hilo lipo katika vyombo vya sheria kwenye ngazi ya Mahakama, hivyo ni vyema kuiachia Mahakama kufanya mamauzi yake ili haki kutendeka.

Awali wananchi wa kijiji hicho, wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu mzozo huo waliitaka Serikali ya Zanzibar kuitumia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), kuchunguza migogoro ya ardhi inayojitokeza kwa wawekezaji ili kupunguza migogoro hiyo.

Walisema wanaamini katika migogoro hiyo kuna harufu kubwa ya rushwa hali ambayo husababisha haki kushindwa kupatikana.

Walisema kitendo cha mwekezaji wa Kampuni Feel Good Entertrises, kuzuiwa kuendelea na ujenzi wakati amefuata taratibu zote na awali maamuzi ya Mahakama yalitoka na kuruhusiwa kufanya ujenzi huenda kuna harufu ya rushwa.

Hivyo, waliitaka serikali kukaa pamoja na wawekezaji hao na kuangalia jambo hilo ili kumalizika na kila mmoja kupata haki yake bila ya kuleta madhara.

Freddie Duchi ambaye ni mjenzi wa Kampuni ya Feel Good Enterprises, alisema anashangaa kuona kilichopo kwasababu mwaka jana walizuiwa kuendelea na ujezi wa jengo hilo kutoka mahakamani lakini baadaye Mahakama iliondoa zuio hilo.

Aidha, alisema serikali inaweka mikakati mizuri ya kuvutia wawekezaji lakini hali hiyo inaharibika kutokana na baadhi ya watu wakiwemo viongozi kujiingiza na kuchangia katika migogoro hiyo.

Naye Mwekezaji wa Kampuni ya Feel Good Entertrises, Paulina, alisema kusimamishwa ujenzi wa eneo hilo amepata hasara, lakini anashangaa mwekezaji mwezake ambaye wanazozana katika mgogoro huo akiendelea na biashara.

Jitihada za kumpata mwekezaji mwingine katika mgogoro huo zilishindikana baada ya waandishi wa habari kufika ofisini kwake na kuelezwa kuwa yupo nje ya nchi.



Wanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari JK Nyerere iliyopo Tarime iliyojengwa na Barrick North Mara wakicheza na kuimba kwa furaha kwenye mahafali shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi mgeni rasmi tamasha la vitabu vya fasihi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAMASHA la vitabu vya fasihi simulizi linatarajia kufanyika kwa mara ya kwanza visiwani Zanzibar Oktoba 20 mwaka huu, litafunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo, Mjumbe wa kamati ya kitaifa ya tamasha la vitabu Zanzibar, Ali Saleh, alisema lengo la tamasha hilo ni kuhuwisha fasihi ambayo kwa sasa imelala.

Alisema Zanzibar katika miaka ya nyuma ilikuwa ikitamba katika fasihi simulizi na kuibua magwiji katika eneo hilo, lakini katika kipindi cha miaka 10 yamejitokeza mabadiliko makubwa na kushuka kwa kazi za fasihi ikiwamo utunzi wa vitabu.

Saleh alisema tamasha hilo litawashirikisha magwiji waliobobea katika fasihi akiwamo mshindi wa Tuzo ya Fasihi ya Nobel, Professa Abdulrazak Gurnah ambaye atachambua kitabu chake kilichompatia heshima kubwa duniani.

Aidha, alisema tamasha hilo pia litawakutanisha waandishi wakongwe ambao watapata nafasi ya kubadilisha mawazo na vijana wanaochipukia katika fasihi.

Mjumbe huyo aliwataja magwiji wengine watakaoshiriki katika tamasha hilo ambao walіwahi kutamba na kutunga vitabu mbalimbali maarufu katika Afrika Mashariki vilivyojikita katika fasihi simulizi ni Professa Said Ahmed Mohamed ambaye alitunga vitabu na mashairi 67 ikiwamo kitabu maarufu cha Asali Chungu. Aidha, alimtaja Mohamed Said Abdalla pamoja na Shafi Adam Shafi aliyetunga kitabu cha Kuli ambacho katika miaka ya 1981 kilitumika kwa wanafunzi wa kidatu cha nne kufanya mitihani ya kiswahili sanifu.

"Lengo la tamasha hili ni kurudisha ari ya utunzi wa vitabu katika fasihi simulizi baada ya kuyumba kwa taaluma hiyo kwa kiasi kikubwa na hivyo vijana kupoteza ari ikiwemo ya kutunga vitabu pamoja na kuwakutanisha magwiji waliobeba katika eneo hilo kuja na kutoa elimu kwa vijana," alisema.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu ya Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Mariyam Jaffar Ismail, alisema fasihi simulizi mchango wake ni mkubwa katika maendeleo ya taifa ikiwamo sekta ya utalii katika kukuza lugha ya Kiswahili kwa wageni.

Naye Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu Huria, Tawi la Zanzibar, Dk. Salma Omar Hamadi, alisema tamasha hilo litaamsha ari katika uandishi wa vitabu pamoja na usomaji wake ambao umeshuka sana.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), DK. Saade Said Mbarouk alisema Zanzibar imejipanga kurudisha hadhi ya fasihi simulizi, kwamba tamasha hilo ni fursa nyingine adhimu ambapo watu watashuhudia kuzinduliwa kwa vitabu mbalimbali vya fasihi.

## Wataalamu afya watakiwa kutoa taarifa za afya ya uzazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amewataka wataalamu sekta ya afya kuendelea kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari katika kutoa taarifa sahihi kuhusiana na masuala ya afya ya uzazi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuvunja ukimya na taarifa hizo kuwafikia vijana ili kujikinga na madhara yanayoweza kuwapata kutokana na kukosa elimu ya masuala hayo.

Dk. Mzuri aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa wadau wa habari na wataalamu wa afya wenye lengo la kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mradi wa utetezi wa masuala ya afya ya uzazi kwa kutumia vyombo vya habari.

Alisema ili kufikisha elimu sahihi ni lazima kuweka na kuripoti takwimu za masuala hayo, ikiwemo vifo vya mama na watoto, mimba za ututoni.

Aidha, alisema elimu ya afya ya uzazi inahitajika tokea katika ngazi ya chini shuleni ili wasichana na wavulana kuwa na elimu ambayo itasaidia kuepukana na mihemko ambayo itasababisha kupata mimba za utotoni.

Naye Ofisa Ufuatiliaji na Taththmini TAMWA, Abdul-Rahman Mohammed, alisema inatekeleza mradi wa utoaji wa elimu ya afya ya uzazi ambapo huwatumia waandishi wa habari kutoa elimu hiyo kupitia vyombo vya habari.

Ofisa Msimamizi wa mradi huo, Zaina Mzee alisema wamewajengea uwezo waandishi wa habari kuifahamu elimu hiyo na kuwasaidia kuandaa vipindi na habari za uchambuzi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, juu ya mabadiliko ya tabia na afya ya uzazi.

Daktari kutoka Wilaya ya Kati Unguja, Amina Hussein, aliwapongeza waandishi wa habari kwa uthubutu wa kuibua changamoto mbalimbali ambazo tayari zimepatiwa ufumbuzi.

Mwandishi wa habari, Salim Said, aliwaomba wataalamu wa afya kuwa wepesi wa kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa na takwimu pindi zinapotakiwa ili kuwezesha waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

# Zungu atoa angalizo ujazo mitungi ya gesi

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Spika, Musa Azzan Zungu ameutaka Wakala wa Vipimo (WMA) kufanya ukaguzi wa ujazo wa mitungi ya gesi ili kuhakiki ujazo wake kuepusha wananchi kuibiwa.

Aliagiza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa utiaji saini mkataba baina ya wakala na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuhusu kutoa mafunzo ya uanagenzi.

Alisema WMA tangu kuanzishwa kwake imekuwa inafanyakazi nzuri, lakini inapaswa kuweka mkazo zaidi kwenye kuhakikisha wananchi hawapunjwi kwenye vipimo.

"WMA mnafanyakazi kubwa na muhimu kwa nchi yetu hongereni sana, lakini bado hamjitangazi, hatuwaoni mkijinadi kuonesha jamii kwamba mpo ili hata wale wavunjifu wa sheria wanaochezea vipimo waone kwamba tukivunja sheria tutapata matatizo.

"Nilimwuliza Mkurugenzi wa WMA hapa kama mna vipimo vya ujazo wa gesi, akasema wanavyo. Sasa mbona hamjitangazi? Tangazeni mazuri mnayofanya dunia nzima ijue mambo mnayofanya," aliagiza.

Alisema uhakiki wa mitungi ya gesi ni muhimu kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanaweza kufanya udanganyifu kama watajua kwamba WMA haifanyi ukaguzi wa mitungi hiyo.

"Kama hatua zinachukuliwa na wenye mitungi wanajua kwamba watu wa WMA wanaweza kupita kukagua, wanaojaza mitungi wataogopa kuweka ujazo mdogo kwa sababu watajua kuna mamlaka ya kuwadhibiti," alisema Zungu.

Pia alipongeza ushirikiano huo akisema anaamini utakuwa wa manufaa kwa pande hizo mbili na kwa maslahi mapana ya taifa na kuwataka kushirikiana kwa maslahi ya taifa.

Alizitaka mamlaka zinazohusika kuchukua hatua kukagua ujazo wa bidhaa zinazofungashwa ili kuangalia thamani ya fedha kwa kuwa baadhi ya bidhaa zinaandikwa ujazo tofauti na uliomo ndani ya bidhaa husika, hivyo kuwapunja walaji.

Zungu aliwataka wataalamu wa vipimo nchini kuwa na nidhamu ya kazi na wasishirikiane na wafanyabiashara kuharibu viwango vya vipimo kwa kuwa wakifanya hivyo, hata elimu yao haitakuwa na maana tena.

Alisema wataalamu hao watakapokuwa CBE watafundishwa kuhusu aina za mafuta yakiwamo ya ndege na namna ya kuyakagua kama yamekidhi viwango.

"Kuna wakati ndege iliangukа kitu cha kwanza wataalau walichukua ni mafuta kwenda kuyapima kama yana viwango. Kwahiyo, tunawataka na ninyi mkawe makini na masomo," aliagiza.

Aliwataka CBE na WMA kufika ofisini kwake kupata suluhisho la changamoto mbalimbali watakazokabiliana nazo kwa kuwa ofisi yake imekuwa inasaidia kukwamua matatizo mbalimbali kwenye jamii.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa, alisema ushirikiano na CBE, umekuwa wa manufaa kwa muda mrefu kwa kuwa ofisi yake imekuwa inaajiri vijana wengi waliotoka chuo hicho.

Alisema CBE na WMA ni watoto wa baba mmoja na mama mmoja kwa kuwa wote wako chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, hivyo CBE imekuwa na wajibu wa kuzalisha wataalamu ambao wanachukuliwa na taasisi mbalimbali ikiwamo WMA.

Alisema WMA ina jukumu la kuhakiki vipimo na kuhakikisha vinatumika kwa usahihi ili wananchi wasipunjwe wanapokwenda kununua bidhaa mbalimbali.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bayport, John Mbaga (kushoto), akikabidhi sehemu ya msaada wa kompyuta 30 kwa Diwani wa Kata ya Kighare, Innocent Mshemo, zilizotolewa na kampuni hiyo kama sehemu ya mkakati wake wa Utawala wa Kijamii na Mazingira (ESG) kuboresha elimu katika shule za Tanzania. Hafla hiyo fupi ilifanyika katika shule za sekondari za Kighare na Kamwala za Mwanga, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara wakubwa wahakikishiwa mkopo wa hadi bilioni 300/- kwa mteja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imewahakikishia wafanyabiashara wakubwa Kanda ya Dar es Salaam wanaohudumiwa na taasisi hiyo, kuwa iko imara kifedha kukopesha mteja mmoja zaidi ya Sh. bilioni 300 kutokana na kukua kwa mtaji wake unaokaribia kufika Sh. trilioni 11.

Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, Alex Mgeni, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Jukwaa la Wafanyabiashara hao 'NMB Business Executive Network' lililofanyika Dar es Salaam chini ya kaulimbiu ya 'Mtandao Thabiti kwa Ukuaji Endelevu wa Biashara', likishirikisha zaidi ya wateja 100.

Jukwaa hilo la kila mwaka limetumika kunadi bidhaa mpya za benki hiyo sokoni ikiwamo Hati Fungani ya Jamii, kupokea maoni ya wateja hao, huku mada mbalimbali zikitolewa kwa washiriki waliohakikishiwa kuwa ufanisi wa NMB ni uthibitisho kuwa fedha za wateja wote ziko salama.

Akimkaribisha mgeni rasmi wa jukwaa hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, Mkuu wa Idara ya Biashara NMB, Mgeni, alisema benki hiyo imeendelea kukua vyema si tu kimtaji, bali pia mtandao mpana wa matawi, mashine za ATM na mawakala kote nchini tangu walipokutana na mtandao huo mwaka jana.

"NMB inafanya vizuri sokoni, na hii maana yake ni kuwa ufanisi wetu ni uthibitisho tosha kuwa fedha zenu, zikiwamo za wateja wengine wadogo na wa kati ziko salama. Tumeimarisha pia ushirikiano wetu na serikali kwa kutoa kupitia Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI).

"Mwaka jana tulikutana hapa tukiwa na mtaji - kwa maana ya mali za benki zilikuwa na thamani ya zaidi Sh. trilioni 9, leo tunakutana tena huku mtaji wetu ukiwa ni zaidi ya Sh. trilioni 10 na tunakaribia Sh. trilioni 11," alisema Mgeni mbele ya Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omar Kumbilamoto.

Alibainisha kuwa faida mojawapo benki inapokuza mtaji, inaweza kuzihudumia kampuni kubwa zinazofanya biashara kubwa Tanzania, ambapo kwa vigezo vya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na kwa mtaji iliyonao NMB inaweza kukopesha hadi Sh. bilioni 300 hadi 350 kwa mteja mmoja.

"Kwa kanuni za BoT, tunaruhusiwa kukopesha chini ya asilimia 25 ya mtaji wetu, ambapo faida moja kubwa ukikopa ndani, gharama inakuwa ndogo na uzalishaji unakuwa mkubwa na bidhaa zitapatikana sokoni kwa bei nafuu, kulinganisha na mikopo inayochukuliwa nje ya nchi na kampuni zenu.

"Kwa hiyo, ni vyema tunapokuza mtaji na kutanua wigo wa ukopeshaji wafanyabiashara wakubwa kwa ustawi wa biashara zao na unafuu wa bei za bidhaa, tunayafanya haya yote huku tukiendelea kutanua mtandao wa matawi yetu kufikia 230, huku tukipanga kufungua matawi sita zaidi," alisema.

Mgeni alibainisha kuwa hivi karibuni wataongeza tawi Kariakoo, ambako wamegundua kuwa matawi yaliyoko yameelemewa na watafungua matawi zaidi jijini Dar es Salaam, ikiwamo Chanika, huku wakitanua mtandao wa mawakala kutoka 21,000 walionao sasa hadi kufikia 30,000 kabla ya mwisho wa mwaka.

Mkuu wa Wilaya Mpogolo aliwashukuru wafanyabiashara wakubwa na wateja wote wa NMB kwa ujumla, akisema mafanikio chanya ya benki hiyo yametokana na uhusiano mwema baina ya pande tatu - yani wateja, serikali na NMB.

# Mtanzania aliyewekeza Thailand kujenga kiwanda cha nguo nchini

**Na Frank Monyo**

MFANYABIASHARA Mtanzania Suleiman Kilonda anayemiliki kiwanda cha nguo jijini Bangkok, Thailand, ameonesha nia ya kujenga kiwanda kikubwa cha nguo nchini kitakachoajiri Watanzania 2,500 na kuzalisha nguo 100,000 kwa siku.

Kilonda hivi karibuni alitunikiwa tuzo ya heshima na Wizara ya Madini baada ya ujumbe ulioongozwa na wizara hiyo kufanya ziara Thailand na kufika katika kiwanda chake cha SK Export kutambua mchango wake kwa kupaisha madini ya Tanzania kupitia nguo anazotengeneza.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Kilonda alisema malengo yake ni kufungua kiwanda kikubwa Tanzania chenye uwezo wa kuajiri Watanzania wengi na kutumika kama sehemu ya kujifunza kwa kila Mtanzania mwenye ndoto za kumiliki kiwanda cha nguo.

"Ombi langu kwa serikali ni kuniwezesha kufikia ndoto hiyo ambayo itawasaidia Watanzania wenzangu kupitia mimi," alisema Kilonda.

Alibainisha kuwa mbali na kumiliki kiwanda, pia amefungua maduka ya kuuza nguo za aina mbalimbali zenye chapa zake, akiajiri wafanyakazi wapatao 200.

Ofisa Mipango Miji kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Michael Majebele, alimpongeza Mtanzania huyo na kueleza kuwa mipango yake ya uwekezaji ni mizuri yenye tija kwa taifa, kuanzia kwenye ajira, kodi na kubadilishana ujuzi.

Majebele alizungumza hayo alipotembelea kiwanda hicho jijini Bangkok na kumweleza kuwa TIC inamkarinisha ili asajili mradi wake, jambo ambalo litamwezesha kufurahia vivutio vya uwekezaji vinavyotolewa nchini ambavyo vitamsaidia kupunguza gharama za uanzishaji kiwanda chake.

## HABARI KIMATAIFA/KITAIFA

# Wapalestina 2,220 wauawa mashambulizi ya Israel

**JERUSALEM,** Israel

WIZARA ya Afya ya Gaza imesema mashambulizi ya Israel katika ukanda wa Gaza yameshawaua zaidi ya watu 2,200 tangu Hamas ilipovamia Israel wiki moja iliyopita. Kati yao, watoto ni 724 na wanawake 458.

Takwimu hizo zilitolewa baada ya taarifa ya awali iliyosema kuwa watu wasiopungua 324 wameuawa katika saa 24 zilizopita kutokana na mashambulizi yanayoendelea.

Taarifa hiyo pia ilitolewa wakati jeshi la Israel likisisitiza tena kuwa wakazi wa Gaza ni lazima waondoke katika eneo la kaskazini la mji huo kabla ya kuanza kwa mashambulizi.

Kauli hiyo imetolewa na Msemaji wa Jeshi la Israel (IDF), Richard Hecht ambaye alieleza kuwa kuna muda salama wa kuondoka kwenye mji huo kati ya saa nne asubuhi na saa 10 jioni kuelekea katika Pwani ya Gaza, ambako kuna umbali wa takribani Km 40.

Hecht alisema wanajua itachukua muda kwa wakazi hao kuhama, lakini wamewashauri wasikawie kuondoka. Njia mbili salama zimetengwa ili kuwaruhusu zaidi ya wakazi milioni 1.1 wa Gaza kuondoka kuelekea kusini mwa ukanda huo.

Maelfu ya wakazi hao wameonekana wakiwa wamejaa kwenye mabasi, magari na mikokoteni ya punda wakilikimbia eneo la kaskazini.

Israel inatarajiwa kuanzisha operesheni ya ardhini dhidi ya kundi la Hamas lililoshambulia kusini mwa Israel Oktoba 7 mwaka huu, huku Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na Ujerumani, pamoja na nchi nyingine kadhaa, huichukulia Hamas kuwa kundi la kigaidi.

### ANGUKO LA HAMAS

Wakati juhudi hizo za kufungua mpaka huo zikiendelea, Jeshi la Israel limesema limefanikiwa kumuua Ali Qadi, Kamanda wa Hamas aliyeongoza vikosi vilivyowaua raia katika shambulizi la ghafla la wiki iliyopita kusini mwa Israel.

Taarifa ya jeshi hilo imesema ndege yake ya kijeshi ilimuua Qadi wa kikosi cha Nukhbha cha Hamas bila kutaja mahali na muda aliouawa.

Taarifa zote za Ofisa wa Palestina na ya Jeshi la Israel zilisema kuwa kamanda huyo alikuwa mmoja wa zaidi ya wafungwa 1,000 wa Palestina walioachiwa huru na Israel mwaka 2011 baada ya Palestina kumwachilia mwanajeshi wa Israel Gilad Shali aliyekamatwa na Hamas mwaka 2006.

Qadi alikamatwa na Israel mwaka 2005 kwa tuhuma za kumteka nyara na kumuua mwanamume wa Kiisraeli aliyetambuliwa kama wakala wa shirika la usalama wa ndani wa Israel, Shin Bet.

Kando ya Qadi, Israel ilisema pia kupitia mashambulizi yake imewaua Ali al Kadhi na Merad Abu wanaoshukiwa kuhusika na shambulio la Hamas lililofanywa kusini mwa Israel Oktoba 7 mwaka huu.

Khadi alikuwa mfungwa aliyeachiliwa na Israel katika makubaliano ya kubadilishana wafungwa mwaka 2005. Alirejea katika ukanda wa Gaza.

### MSAADA WAWASILI MISRI

Wakati huo, ofisa mmoja wa shirika la hilali nyekundu alisema kuwa ndege zilizobeba misaada zimewasili katika rasi ya Sinai ambako misaada imekuwa ikizuiwa mpaka itakapopatikana njia salama ya kuifikisha karibu na ukanda wa Gaza.

Misri ilisema sehemu ya upande wake wa mpaka wa Rafah unaoiunganisha Sinai na ukanda wa Gaza inasalia kuwa wazi ingawa usafiri umezuiwa kwa siku kadhaa kutokana na mashambulizi ya Israel yanayoelekezwa kwenye upande wa mpakani mwa Palestina. **DW**




Watu waliobeba mabango na bendera za Palestina wakifanya maandamano mjini London yakilenga kuunga mkono Wapalestina. **PICHA: MTANDAO**

## Bajaji za wenye ulemavu kuruhusiwa kuingia mjini

**Na Restuta James**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, amesema serikali inaandaa utaratibu wa kuweka alama ya utambuzi na namba maalum kwenye bajaji zinazoendeshwa na watu wenye ulemavu ili ziingie katikati ya jiji.

Mpogolo alibainisha mpango huo mwishoni mwa wiki wakati wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Walemavu Waendesha Bajaji Dar es Salaam (UWAWABADA).

Alisema uamuzi huo unatokana na kikao cha kamati ya usalama barabarani, lakini bado suala hilo linasubiri baraka za vikao vingine kisha kutungiwa sheria ndogo ili kuliweka kisheria.

"Tunaweka alama na namba ili yeyote atakayeingia katikati ya mji, mtajua huyu si mwenzenu... hivyo niwaombe mnapokuwa mnajadili na kuazimia wekeni na utaratibu wa nini kifanyike kwa atakayekwenda kinyume cha maazimio yenu," alisema Mpogolo.

Pia alitoa onyo kwa wale watakaobainika kuchukua bajaji za wenye ulemavu na kuziendesha katika maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya walemavu ilhali wao wakiwa si walemavu. Sheria itachukua mkondo wake.

Mpogolo alikuwa akijibu ombi la UWAWABADA kuhusu kuwaruhusu kuingiza bajaji katikati ya mji pamoja na kuwapa maegesho tofauti na wengine.

Ombi hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA), Hamad Komboza, mbele ya Mpogolo, aliyekuwa mgeni rasmi, kwenye Mkutano Mkuu wa UWAWABADA uliokuwa na lengo la kusikiliza changamoto zao.

# Mashindano ya baiskeli kuhamasisha uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

YAKIFANYIKA kwa mwaka wa nne sasa, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amesema mashindano ya mbio za baiskeli yanayoandaliwa na Benki ya CRDB mkoani humu, yamesaidia kuutangaza mkoa huo na kufungua zaidi fursa za kiuchumi na uwekezaji.

Mndeme alisema juzi wakati wa kilele cha Mbio za Baiskeli za CRDB Shinyanga (Shinyanga CRDB Cycling Rally), akisema si tu zinatoa fursa kwa wananchi wanaoshiriki kuimarisha na kulinda afya zao, bali washindi wanapata zawadi zinazowahamasisha wao na wengine kuendelea kushiriki mbio hizo.

Baada ya mbio hizo kufanyika kwa mafanikio kwa miaka minne sasa, alisema iwapo utafiti utafanyika leo, hatoshangaa akisikia Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa idadi kubwa ya baiskeli, jambo litalokuwa limechangiwa na benki hiyo.

"Mbio hizi zimetoa fursa ya kutangaza mkoa wetu pamoja na kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi na wafanyabiashara.

"Kadri miaka inavyozidi kwenda, umaarufu wa mbio hizi unazidi kuongezeka. Hivyo basi, wakati Benki ya CRDB ikifungua njia, ninaziomba kampuni nyingine nazo kuangalia namna ya kufungua fursa za mkoa wetu huu, jambo litakalosaidia kuboresha maisha ya wananchi," alisema Mndeme.

Endapo mbio hizo zitaendelezwa na kuwakaribisha washiriki kutoka kote nchini hata nje ya mipaka ya Tanzania, Mndeme alisema anaamini zitaitangaza vyema Shinyanga na kutoa fursa kwa vijana kushiriki mashindano ya aina hiyo kimataifa na kuimarisha kipato chao.

Kabla ya kuhitimishwa kwa mbio hizo, zilitanguliwa na shughuli za kijamii ikiwamo kuchangia damu ambapo zaidi ya chupa 500 za damu salama zilikusanywa kwa ajili ya wagonjwa wenye uhitaji wanaotibiwa katika hospitali na vituo vya afya mkoani humu na nchini kote kwa ujumla.

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Magharibi, Jumanne Wagana, alisema mbio hizo hufanyika kila mwaka Siku ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ambaye alipenda kila mwananchi kuwa huru kiuchumi kwa kujituma kufanya kazi kulingana na fursa zilizopo kwenye eneo alilopo.

Mbali na mbio hizo za baiskeli, Benki ya CRDB pia huandaa na kusimamia mbio za kimataifa zijulikanazo kama CRDB Bank Marathon huku ikidhamini mingine kadhaa zikiwamo jezi za Zanzibar Heroes, Simba Day na Wiki ya Mwananchi, pia ni mfadhili wa Klabu ya Namungo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na inadhamini Mashindano ya CRDB Bank Ngalawa Race yanayofanyika Kizimkazi, visiwani Zanzibar.

# MBRAZIL KIBOKO YA YANGA ATUA KUINOA SINGIDA FG

**Na Saada Akida**

HATIMAYE Klabu ya Singida Fountain Gate, imemtambulisha rasmi kocha mkuu mpya kutoka nchini Brazil, Ricardo Ferreira, ikimpa mkataba wa mwaka mmoja kukinoa kikosi cha timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara huku akitamba amewahi kuipiga Yanga ndani nje michuano ya kimataifa.

**Ferreira anaenda kuchukua nafasi ya aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Ernst Middendorp ambaye aliondoka kwa madai ya kuingiliwa majukumu yake na viongozi wa klabu hiyo.**

Kocha huyo amekuja na msaidizi wake ambaye ni Andrews Barbosa, wakisaidiwa na makocha waliopo ndani ya benchi la ufundi kuhakikisha timu Singida FG inafikia malengo yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Olebile Sikwane, alisema baada ya kucheza mechi tano bila ya kuwa na kocha mkuu, sasa wanamtambulisha rasmi Ricardo kuwa kocha mkuu wa timu hiyo kwa mwaka mmoja.

Alisema wamempa mkataba wa mwaka mmoja wenye kipengele cha kuongeza hapo baadaye atakapofikia malengo yao na wana imani kubwa na kocha huyo kuifikisha mbali timu hiyo.

"Baada ya kukaa miezi kadhaa bila kocha mkuu, bodi imeona kutafuta kocha mwingine kwa sababu Singida Fountain Gate FC ipo kwenye ushindani wa ligi, kwa haraka tukaingia sokoni kutafuta na hatimaye tumeingia makubaliano na Ricardo.

"Tumeingia makubaliano na Ricardo baada ya kuridhishwa na CV zake, tunaimani atatufikisha katika malengo tunayotarajia kufikia kwenye ligi," alisema Sikwane.

Naye kocha Ricardo alisema anataka kufanya kitu tofauti na makocha waliopita, akidai kuanzia sasa itakuwa ngumu mno kuifunga Singida Fountain Gate FC na itakuwa tishio kama ilivyo kwa timu za Simba na Yanga.

Alisema ana uzoefu mkubwa wa soka la Afrika na atahakikisha muda mfupi atakaokuwa ndani ya benchi hilo, atakuwa amefanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi cha Singida Fountain Gate.

"Ninafahamu vizuri soka la Afrika kwa sababu nimewahi kufundisha timu nyingi za Afrika, pia katika kumbukumbu zangu miaka ya 2006 au 2007 nimewahi kumfunga Yanga nje, ndani nikiwa na klabu ya Al Hilal ya Sudan.

Timu kocha huyo alizowahi kuzifundisha ni pamoja na Klabu ya Al Hilal ya Sudan mwaka 2006 hadi 2008, Ismaily ya Misri 2008 hadi 2009, Al-Ahli ya Doha 2011-2012. Timu zingine alizofundisha ni Al-Merrikh na Al-Ahly Shandi zote za Sudan na kwao Brazil ameinoa Bonsucesso FC ya Rio de Janeiro.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Morogoro, Dk. Rose Rwakatare, akitoa msaada wa jezi na mipira kwa ajili ya timu zinazotarajiwa kuchuana kwenye mashindano ya Rwakatare Cup (Wazazi Cup), hivi karibuni mkoani humo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Tamaduni ya Wamakonde sasa kidigitali*

**Na Mary Geofrey**

UZINDUZI na maonyesho ya mradi wa Uhifadhi wa Tamaduni ya Makonde kwa njia ya kidigitali, utafanyika kwa kuanza kuoneshwa kwenye mitandao ya kijamii ikiwamo Instagram na facebook kupitia vichujio picha 'Instagram filters'.

Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Onastories, kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa, walizindua mpango huo jana jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Onastories ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia halisia, Tulanana Bohela, alisema uzinduzi huo unahusisha mila za kabila la Makonde kutangaza tamaduni zao hasa chale za uso pamoja na uchongaji wa vinyago.

"Kwa kuanzia tumewawezesha wabunifu 12 wenye uwezo na maarifa ya teknolojia ya uhalisia ongezi kwa ajili ya kuhifadhi utamaduni wa Makonde kidijitali.

"Kuchochea ushirikiano kati ya wahifadhi wa utamaduni, wanahistoria, wakusanyaji wa nyaraka na wabunifu ili kuhakikisha uhalisia unakuwapo. Kuweka chale ya Makonde katika mfumo wa kidigitali na kuifanya iweze kupatikana kwa kuhifadhi, kuelimisha, na kuunganisha kwenye majukwaa kama vile Instagram, Facebook, na TikTok," alisisitiza Bohela.

Naye Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Makumbusho ya Taifa, Elvida Max, akizungumza wakati wa uzinduzi huo, alisema mpango huo utadumisha tamaduni vizazi vingi vijavyo.

Alisema kabla ya uzinduzi, taasisi hiyo imefanya maandalizi kwa miezi sita, kufuatilia namna Wamakonde wanavyoishi na kuiweka historia hiyo kwenye mfumo wa kidigitali na baadae kuhifadhiwa makumbusho ya Taifa.

Mradi huu umechochewa na kupotea kwa tamaduni ya uchanjaji chale katika jamii ya Kimakonde, athari za mabadiliko ya kiteknolojia katika ushawishi wa watalii katika makumbusho, na jinsi teknolojia inavyoweza kutumika kuunganisha kizazi cha leo na yale waliyoyafanya wahenga kwa kutumia teknolojia ya uhalisia wa ongezi.

## Mbeya Kwanza FC yapigwa ya kwanza

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza imepoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Championship baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya TMA, mechi ikipigwa juzi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Alikuwa ni beki wa kulia Ally Shomari, aliyefunga bao pekee dakika ya pili tu ya mchezo ambalo lilidumu dakika zote 90 na kuhitimisha rekodi nzuri ya Mbeya Kwanza ambayo ilicheza mechi tano ikishinda nne na sare moja kabla ya kupoteza kwenye raundi ya sita.

Kipigo hicho kinaifanya kuenguliwa kileleni ikishuka nafasi ya pili na kubaki na pointi zake 13, huku TMA ikiongoza ligi kwa kufikisha pointi 14.

TMA ambayo inacheza Ligi ya Championship kwa mara ya kwanza baada ya kupanda kutoka Ligi Daraja la Pili, 'First League', ndiyo timu pekee kwenye ligi hiyo kwa sasa ambayo haijapoteza mechi yoyote mpaka kufikia raundi hiyo.

## Wazazi Cup kuanza kupigwa Morogoro

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Wazazi Cup mkoani Morogoro, ambayo yameandaliwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi mkoani humo, Dk. Rose Rwakatare, yanatarajiwa kutimua vumbi muda wowote kuanzia sasa, imeelezwa.

Mratibu wa Mashindano hayo, Ismail Kifaru, alisema jana kuwa maandalizi yote yamekamilika na timu za wilaya zote zimeshapatiwa jezi na mipira kwa ajili ya kujiandaa kwa mashindano hayo.

Alitaja wilaya zitakazoshiriki mashindano hayo kuwa ni Malinyi, Kilombero, Ulanga, Kilosa, Mvomero, Gairo, Morogoro Mjini na Morogoro Vijijini, ambapo timu zitachuana kuanzia ngazi ya kata na kupata moja itakayowakilisha wilaya kwenye mashindano ya mkoa.

"Maandalizi yanakwenda vizuri timu zote zitakazoshiriki zimeshepewa mipira na jezi ni taratibu chache tu zimebaki kukamilisha maandalizi hayo na kuna zawadi mbalimbali zimeandaliwa kwa mshindi wa kwanza, wapili na wa tatu," alisema mratibu huyo.

Akiwa kwenye ziara yake, Dk. Rose aliwataka viongozi wa jumuiya za chama hicho kuhamasisha michezo kwenye wilaya zao kwani michezo ni muhimu kwa afya na inaimarisha upendo na mshikamano.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA KUMSAJILI SANCHO

BARCELONA wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Jadon Sancho, 23, Juni, mwakani ikiwa wanaweza kukubaliana na dili la bei iliyopunguzwa. Winga huyo wa England pia amehusishwa na uhamisho wa mkopo kwenda Juventus. ***(Sport)***

### ONANA KUREJEA INTER

MTENDAJI Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amekataa kuondoa uwezekano wa mlinda mlango wa Cameroon, Andre Onana, 27, kurejea katika klabu hiyo ya Serie A baada ya kuanza kwa mwenendo usioeleweka kule Manchester United. ***(Mail)***

### GUIMAREZ KUJIUNGA BARCA

BRUNO Guimaraes, 25, ana kipengele katika mkataba wake mpya na Newcastle United ambacho kitamruhusu kiungo huyo wa kati wa Brazil kujiunga na Barcelona kwa ada ya euro milioni 65 hadi 70. ***(Sport)***

### SANE KUMRITHI SALAH

LIVERPOOL imemfanya mshambuliaji wa Ujerumani, Leroy Sane, 27, kuwa mlengwa wao namba moja kuchukua nafasi ya Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, ikiwa Mmisri huyo ataondoka na huenda akavunja rekodi yao ya uhamisho ili kumpata nyota huyo wa Bayern Munich. ***(Mirror)***

### VINICIUS KAMSHAWISHI JUDE

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Brazil, Vinicius Jr, 23, amesema alimtumia ujumbe kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 20, ili kumshawishi atoke Borussia Dortmund na kwenda Bernabeu msimu wa majira ya joto. ***(L'Equipe)***

### PEP SIMU KWA SAA TATU

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, alipiga simu kwa saa tatu Jude Bellingham kabla ya kuhamia Real Madrid kwa nia ya kumshawishi mchezaji huyo wa Kimataifa wa England kujiunga nae. ***(Cadena Ser via Goal)***

### PHILLIPS KUHAMA CITY

KIUNGO Kalvin Phillips, 27, anafikiria kuhama Manchester City Januari kwa kuhofia kukosa muda wa kucheza kunaweza kuzuia nafasi yake ya kujiunga na kikosi cha England chini ya Kocha Gareth Southgate kwenye Euro 2024. ***(Mirror)***

### ROWE AFUATILIWA EPL

KLABU za Aston Villa na Crystal Palace ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu England zinazomfuatilia mshambuliaji wa Norwich na England chini ya umri wa miaka 21, Jon Rowe, 20, ambaye amebakisha miezi 18 katika mkataba wake pale Carrow Road. ***(Mail)***

### ATAKA NAMBA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa England, Charlie Patino, 19, anataka kujihakikishia mustakabali wa muda mrefu katika klabu mama Arsenal wakati muda wake wa sasa wa mkopo kule Swansea utakapomalizika. ***(Mail)***

### MATSEN ATAJWA BARCA

BARCELONA inajipanga kumnunua beki wa kushoto wa Chelsea na Uholanzi, Ian Maatsen mwenye umri wa miaka 21, ambaye alikataa uhamisho wa pauni milioni 32 kwenda Burnley na mkataba wake unamalizika Juni. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO MWANASOKA TAJIRI ZAIDI MWAKA 2023

### ●●● Amwacha mbali Messi na Neymar huku Mbappe, Haaland nao wakiingia...

**NEW YORK,** Marekani

CRISTIANO Ronaldo ndiye mwanasoka anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani kwa mwaka 2023, akiwazidi wachezaji wenzake, Lionel Messi na Neymar katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa mujibu wa Jarida la Forbes la Marekani.

**Ronaldo, ambaye Forbes pia imemworodhesha kama mwanamichezo anayelipwa fedha nyingi zaidi katika mchezo wowote duniani kwa sasa, anaongoza orodha hiyo akiwa na mapato yanayotajwa kuwa ni dola milioni 260.**

Mkataba wa fowadi huyo wa Ureno na Klabu ya Al Nassr ya Saudi Arabia, ambayo alijiunga nayo kutoka Manchester United Januari, unatajwa kuwa wa thamani ya dola milioni 200 huku mkataba wa matangazo ya chapa za Nike na Jacob & Co kwa pamoja yakigharimu dola milioni 60 kwa mwaka kwa mujibu wa Forbes.

Messi yeye anashika nafasi ya pili kwenye orodha hiyo akipata jumla ya dola milioni 135 iliyochochewa na uhamisho wake wa kujiunga na Klabu ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami.

Messi ndiye mchezaji wa kwanza wa MLS kuingia kwenye 10-bora tangu David Beckham mwaka 2012.

Mshambuliaji wa Brazil, Neymar anashika nafasi ya tatu bora akiwa na mapato ya jumla ya dola milioni 112 baada ya kusajiliwa na Al Hilal kwenye Ligi ya Saudia Agosti mwaka huu.

Ushawishi wa Saudi Pro League unaonekana wazi katika orodha ya Forbes huku wachezaji wanne (Ronaldo, Neymar, Karim Benzema na Sadio Mane) wakiwa miongoni mwa wachezaji 11 wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani.

Kwa mujibu wa Forbes, mapato ya wachezaji wanne wa Saudi Pro League kwa pamoja yanahesabu zaidi ya nusu ya dola milioni 995 kwa pamoja iliyopatikana na wachezaji wote 11 kwenye orodha tajiri. Kylian Mbappe anafuata kwenye viwango, akiwa nyuma kidogo ya mchezaji mwenzake wa zamani wa Paris Saint-Germain, Neymar, mwenye mapato ya jumla ya dola milioni 110.

Mchezaji wa Manchester City, Erling Haaland ndiye mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu England akiwa na jumla ya mapato ya kila mwaka zaidi ya yale ya Mohamed Salah wa Liverpool na mwenzake, Kevin De Bruyne wa City.

Forbes ilisema takwimu zake za mapato ya uwanjani ni pamoja na fedha zote za zawadi, mishahara na bonasi zilizopatikana katika kipindi cha miezi 12 wakati mapato ya nje ya uwanja ni makadirio ya mikataba ya udhamini, ada, mapato ya leseni na mapato ya fedha kutoka kwenye biashara wanazozifanya.

**Orodha kamili wanasoka 11 wanaolipwa zaidi mwaka 2023 ya Forbes**

1. Cristiano Ronaldo **(Dola Mil. 260)**
2. Lionel Messi **(Dola Mil. 135)**
3. Neymar **(Dola Mil. 112)**
4. Kylian Mbappé **(Dola Mil. 110)**
5. Karim Benzema **(Dola Mil. 106)**
6. Erling Haaland **(Dola Mil. 58)**
7. Mohamed Salah **(Dola Mil. 53)**
8. Sadio Mane **(Dola Mil. 52)**
9. Kevin De Bruyne **(Dola Mil. 39)**
10. Harry Kane **(Dola Mil. 36)**
11. Robert Lewandowski **(Dola Mil. 34)**

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
EGYPT
VERSUS
ALGERIA
1 | 2.91
X | 3.12
2 | 2.52

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RATCLIFFE KUINUNUA MAN UTD, SHEIKH JASSIM AJITOA



**MANCHESTER,** England

SIR Jim Ratcliffe amekubali dili la kununua hisa asilimia 25 za Manchester United baada ya Sheikh Jassim bin Hamad Al Thani kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kutwaa nafasi hiyo, kwa mujibu wa 90min.

Sheikh Jassim alikuwa akitafuta kutwaa klabu hiyo kwa asilimia 100, akitoa ofa ya kulipa takriban pauni bilioni tano kuchukua udhibiti wa United na pia kuashiria nia ya kulipa madeni ya pauni bilioni moja ya klabu hiyo.

Hata hivyo, familia ya Glazers inayoimiliki klabu hiyo wanaithamini klabu hiyo juu zaidi, labda hadi pauni bilioni 10, na vyanzo vimethibitisha kwamba, Sheikh Jassim alijiondoa kwenye mchakato huo baada ya kukataa kuongeza ofa yake ya hivi karibuni.

Badala yake, makubaliano yamefikiwa na Ratcliffe, ambaye anatazamiwa kupata umiliki wa klabu hiyo kwa asilimia 25.

Ratcliffe anatumaini kupata umiliki kamili wa klabu katika siku zijazo, lakini yuko tayari kuanza na dau la hisa chache ambalo litaiwezesha familia ya Glazers kubakia kwenye umiliki wa asilimia kubwa pale Old Trafford kwa sasa.

The Glazers walikuwa wakisita kuiuza United kwa bei iliyo chini ya bei waliyotakiwa na kumekuwa na sintofahamu kwa muda mrefu kama dili lolote lingekubaliwa huku mazungumzo yakichukua karibu mwaka mmoja.

Lakini Ratcliffe, ambaye ofa yake kwa United iliithaminiwa zaidi na klabu hiyo kuliko ile ya Sheikh Jassim, amekubali kuchukua mbinu polepole zaidi ya kuichukua na ameweza kuwaridhisha familia ya Glazers.

# Alexander-Arnold hajui nafasi yake bor

**LIVERPOOL,** England

TRENT Alexander-Arnold amekiri kuwa hajui nafasi yake bora ya kucheza baada ya kutumia muda katika safu ya kiungo msimu huu.

Kiungo huyo wa kati katika siku zake za akademi, Alexander-Arnold, alifanywa kuwa beki wa kulia na Liverpool, lakini maswali juu ya uwezo wake wa ulinzi yamewafanya Kocha wa Wekundu hao, Jurgen Klopp na wa kikosi cha England, Gareth Southgate, kumtumia mbele zaidi katika safu ya kiungo.

Baada ya kuanza kuelekea mwisho wa msimu uliopita kama mbinu ya kurekebisha kiwango cha klabu, Alexander-Arnold amecheza kama kiungo na pia mwaka huu.

Wote Klopp na Southgate watalazimika kuamua ni wapi mustakabali wa muda mrefu wa Alexander-Arnold upo na mchezaji mwenyewe amekiri kuwa hajui anapaswa kucheza wapi.

"Watu wanaona uwezekano wa mimi kuwa na ufanisi zaidi katikati ya uwanja," alisema.

"Hiyo labda ni njia ya kwenda mbele. Lakini nani anajua? Si uamuzi wangu. Ninaweza kuchezeshwa tu katika nafasi niliyoambiwa.

Akitafakari juu ya uhamisho wake wa awali chini ya Klopp msimu uliopita, Alexander-Arnold aliongeza: "Wakati kocha alinionesha jukumu lililopinduliwa, niliona kama fursa ya kuonesha ninaweza kucheza katikati ya uwanja. Unaweza kupata mchezo mmoja, haifanyi kazi ukiwa umetoka kucheza maisha yako yote katika nafasi ya beki wa kulia.



CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# KOCHA SIMBA ATUA IHEFU

**Na Saada Akida**

KOCHA wa zamani wa Simba raia wa Uganda, Moses Basena, anatajwa kujiunga na Ihefu FC, kuchukua nafasi ya Zuber Katwila aliyefutwa kazi juzi wiki iliyopita.

Basena ambaye aliwahi pia kuwa Kocha Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, alitua nchini majuzi usiku na juzi alifunga safari hadi Mbeya kwa mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Bara.

**Kama dili hilo litakamilika itakuwa ni mara ya pili kwa Basena kufundisha Tanzania baada ya kuifundisha Simba mwaka 2011, kabla ya kuachana nao na kwenda kwao Uganda.**

Taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jana kutoka ndani ya timu hiyo, Basena yuko Mbeya kwa ajili ya kufanya mazungumzo na uongozi wa Ihefu FC na mambo yakienda sawa atachukuwa nafasi ya Katwila.

Mtoa habari wetu, alisema awali viongozi wa Ihefu walimtaka Seleman Matola pamoja na wasaidizi wake kutoka kikosi cha timu ya Vijana ya Simba, lakini klabu hiyo iliweka ngumu na baada ya kushindikana wakaangukia kwa Basena.

“Kama mambo yataenda vizuri, Basena atatangazwa rasmi kuwa kocha mkuu wa Ihefu FC, tayari yuko hapa nchini na ameshaenda Mbeya kwa ajili ya mazungumzo hayo,” alisema mtoa habari wetu ndani ya klabu hiyo.

Kupitia Ofisa Habari wa timu hiyo, Peter Endrew, alisema mchakato wa kutafuta kocha mwingine unaendelea na wataweka wazi baada ya kukamilika kwa mchakato huo.

## Polisi Jamii Cup yazinduliwa Dar

**Na Frank Monyo**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani (Trafki), kwa kushirikiana na Serengeti Breweries Limited (SBL), kupitia chapa yake ya Serengeti Premium Lager, wamezindua rasmi mashindano ya mpira wa miguu 'Usalama Barabarani Jamii Cup 2023' kwa waendesha pikipiki maarufu bodaboda wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mashindano hayo yatashirikisha waendesha pikipiki kutoka ngazi za kata hadi kitaifa, ambapo yataenda sambamba na kutoa elimu ya usalama barabarani pia yatasaidia kuibua vipaji vya mpira wa miguu.

Akizindua mashindano hayo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, Kamishna wa Polisi, Faustine Shillogile, alisema polisi haipo tu kwa ajili ya kuadhibu, bali pia kutoa elimu kwa raia wa Tanzania.

Alisema ushirikiano huo umepangwa kushirikisha waendesha pikipiki wenye shauku katika ngazi zote za mashindano, kuanzia ngazi ya kata hadi ya taifa kwa kuwakutanisha kupitia michezo sambamba na kupewa elimu.

Aliongeza kuwa madereva watakaojifunza mafunzo ya msingi kutoka SBL kupitia Kampeni ya Inawezekana wanapaswa kuzingatia maarifa yatakayotolewa na kuyatekeleza kwa kuwajibika wanapotumia vyombo vya moto kwa usalama wa watu wengine.

Meneja Mawasiliano na Uendelevu wa SBL, Rispa Hatibu, alisema kuwa imani ya kampuni hiyo ni kwamba kunywa kwa uwajibikaji ni jukumu la mtu binafsi, ambapo SBL inaamini kwa dhati kwamba kunywa kwa uwajibikaji huanzia kwa mtu. Inajumuisha kufanya uchaguzi wenye msingi kuhusu unywaji wa pombe na kuelewa matokeo ya matendo ya mtu barabarani na katika jamii.

Alisema Kampeni ya Inawezekana inalenga kukuza na kuhamasisha tabia ya unywaji pombe kwa kuwajibika na usalama barabarani katika jamii yetu.



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini kujiandaa na mechi yao ijayo dhidi ya Azam FC, itakayopigwa Jumapili wiki hii. **PICHA: YANGA**

## *Robertinho aanika mfumo*

INATOKA UKURASA 24

kutoka kwenye benchi la ufundi pamoja na madaktari,” alisema.

Alisema pamoja na yote, maendeleo ya kipa huyo yanampa uhakika wa kuwa na nguvu mpya kwenye eneo la langoni na hasa katika mechi ya marudiano nchini Misri, kwani hata kama ikitokea hakucheza Dar, inawezekana kabisa akawa langoni mechi ya marudiano.

Robertinho alisema mchezaji mwingine aliyekuwa majeruhi Henock Inonga kwa sasa hana tatizo lolote na moja kwa moja atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Al Ahly.

Inonga ambaye aliumia Septemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, alipokanyagwa na mchezaji wa Coastal Union, Haji Ugando kwa sasa yupo na kikosi cha Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kwa mujibu wa Robertinho amepona na hana tatizo lolote.



## MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 16/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2606 | Diagoras FC vs Kissamikos | 3.61 | 3.15 | 1.98 |
| 13:30 | 4347 | SC Poltava vs Yarud Mariupol | 1.95 | 3.37 | 3.32 |
| 14:30 | 2198 | China vs Uzbekistan | 3.37 | 3.21 | 2.21 |
| 15:00 | 3674 | Charlton U23 vs Millwall U21 | 3.25 | 4.27 | 1.79 |
| 16:00 | 2076 | FK Mladost Gat vs FK Graficar Beograd | 1.85 | 3.32 | 3.72 |
| 16:00 | 2439 | FK Radnicki Sremska Mitrovica vs FK Odzaci | 2.52 | 2.83 | 2.78 |
| 16:00 | 4113 | Fleetwood Town Reserve vs Birmingham U21 | 2.04 | 4.18 | 2.70 |
| 16:00 | 5058 | OFK Vrsac vs FK Novi Sad | 1.53 | 3.69 | 5.46 |
| 17:00 | 4479 | CA Independiente W vs CA Banfield | 1.77 | 3.50 | 3.70 |
| 17:00 | 5823 | Ferro Carril Oeste vs CA Estudiantes de Caseros | 2.22 | 3.22 | 2.96 |
| 18:00 | 3950 | Mozambique vs Nigeria | 9.07 | 4.43 | 1.38 |
| 18:00 | 5013 | Mjondalen 2 vs Odds BK 2 | 2.73 | 4.24 | 1.97 |
| 19:00 | 1114 | Egypt vs Algeria | 2.91 | 3.12 | 2.52 |
| 19:00 | 2036 | Azerbaijan vs Austria | 8.01 | 4.74 | 1.38 |
| 19:30 | 3893 | Ukraine U21 vs England U21 | 5.48 | 3.96 | 1.50 |
| 20:00 | 2040 | Viking FK 2 vs Eiger | 1.09 | 8.45 | 14.08 |
| 20:30 | 1414 | Rosenborg BK 2 vs Verdal | 1.56 | 4.30 | 4.10 |
| 20:30 | 1724 | MSV Duisburg W vs Essen-Schonebeck W | 3.56 | 3.41 | 1.90 |
| 21:00 | 1871 | IA Sud America vs Club Oriental De Football | 2.51 | 2.89 | 2.74 |
| 21:30 | 1008 | Potenza SC vs Torre Neapolis | 2.01 | 3.40 | 3.61 |
| 21:30 | 1088 | Senegal vs Cameroon | 2.19 | 3.21 | 3.42 |
| 21:30 | 1130 | Patronato Parana vs Agropecuario | 4.51 | 3.38 | 1.72 |
| 21:30 | 1661 | Defensores Belgrano vs San Martin Tucuman | 2.43 | 2.95 | 2.86 |
| 21:30 | 2152 | CA Guemes vs Club Almagro | 1.92 | 3.09 | 3.93 |
| 21:30 | 3295 | Northern Ireland U21 vs Serbia U21 | 4.77 | 3.60 | 1.63 |
| 21:30 | 3568 | Estudiantes Rio Cuarto vs Nueva Chicago | 1.89 | 3.10 | 4.03 |
| 21:30 | 3923 | Gimnasia Mendoza vs Guillermo Brown | 1.39 | 3.92 | 7.85 |
| 21:30 | 4225 | CA Acassuso vs Argentino De Quilmes | 1.97 | 3.11 | 3.72 |
| 21:30 | 4335 | Almirante Brown vs Temperley | 1.73 | 3.24 | 4.71 |
| 21:30 | 4868 | Deportivo Moron vs San Telmo | 1.59 | 3.67 | 5.09 |
| 21:30 | 5275 | Flandria vs San Martin SJ | 3.25 | 3.30 | 2.05 |
| 21:30 | 5785 | Atletico Alvarado vs Defensores Unidos | 2.03 | 2.99 | 3.67 |
| 21:45 | 1167 | Iceland vs Liechtenstein | 1.08 | 9.51 | 36.98 |
| 21:45 | 1232 | Pontedera vs Rimini | 2.09 | 3.30 | 3.46 |
| 21:45 | 1486 | Casertana vs Avellino | 2.88 | 2.93 | 2.62 |
| 21:45 | 3597 | Greece vs Netherlands | 3.69 | 3.27 | 2.07 |
| 21:45 | 4686 | Luxembourg vs Slovakia | 3.33 | 3.22 | 2.23 |
| 21:45 | 4775 | Gibraltar vs Ireland | 30.67 | 8.46 | 1.10 |
| 21:45 | 4820 | Bosnia and Herzegovina vs Portugal | 5.70 | 4.01 | 1.57 |
| 21:45 | 5250 | Belgium vs Sweden | 1.67 | 3.80 | 5.07 |
| 21:45 | 5795 | Pescara Calcio vs Vis Pesaro | 1.46 | 4.39 | 6.27 |
| 22:00 | 2001 | Russia vs Kenya | 1.66 | 3.80 | 5.17 |
| 22:00 | 3299 | Levante vs Racing Ferrol | 1.79 | 3.38 | 4.27 |
| 22:00 | 5599 | Banfield vs Atletico Tucuman | 2.16 | 2.95 | 3.36 |
| 23:30 | 3366 | Universitario Popayan vs Fortaleza (COL) | 4.03 | 3.01 | 1.93 |

### JUMANNE - 17/10/2023


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1262 | Leones FC vs Real Cartagena | 2.06 | 3.31 | 3.21 |
| 02:00 | 1665 | French Guiana vs Saint Vincent and the Grenadines | 1.32 | 4.79 | 7.34 |
| 03:00 | 5684 | Dominican Republic vs Barbados | 1.16 | 6.54 | 12.27 |
| 07:45 | 4334 | Guam vs Singapore | 7.95 | 4.69 | 1.31 |
| 10:00 | 5621 | Mongolia vs Afghanistan | 3.30 | 3.15 | 2.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 16, 2023

Nipashe

Ronaldo mwanasoka tajiri zaidi 2023 UKURASA 21

# Robertinho aanika mfumo wa kuishika Al Ahly AFL

## ●●● Ngoma, Mzamiru wahusika huku Chama, Kibu nao wakitakiwa kuhakikisha...

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajiwa kushuka dimbani Ijumaa ijayo kucheza mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League dhidi ya Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri, Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi hao, Robertinho Oliveira, ameanika mfumo anaouandaa ili kuwashika wapinzani wao hao, huku akiweka wazi haitakuwa mechi rahisi.

**Michuano hiyo inayoshirikisha Klabu nane bora zaidi barani Afrika, ambazo ni Al Ahly (Misri), Wydad Casablanca (Morocco), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Esperance Tunis (Tunisia), Simba (Tanzania), Petro Atletico de Luanda (Angola), Enyimba FC (Nigeria) na TP Mazembe (DR Congo), itaanza Ijumaa wiki hii kwa mechi ya ufunguzi kupigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Pia michuano hiyo itachezwa kwa mtindo wa mtoano nyumbani na ugenini ambapo baada ya mechi hiyo ya Ijumaa, Simba itashuka tena dimbani ugenini dhidi ya Al Ahly Jumanne ya wiki ijayo nchini Misri na mshindi wa jumla atatinga nusu fainali.

Akiuzungumzia mchezo huo, Robertinho alisema anafahamu itakuwa ngumu kwa sababu Al Ahly ina uzoefu wa mechi nyingi za kimataifa na kwa aina ya uchezaji wao anatengeneza mfumo wa kukabiliana nao.

"Natakiwa kuwa makini kutengeneza mfumo kwenye eneo la katikati, viungo wakabaji na viungo washambuliaji ndiyo hapo tunaweza kukabiliana nao, ila naamini tutafanya vizuri kutokana na mwenendo tunaokwenda nao kwenye Ligi Kuu na tulioonesha katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mashabiki wawe na imani kwa sababu timu inaendelea kutengenezwa na tayari kila mtu anaona imeshaanza kuimarika," alisema Robertinho.

Katika eneo la safu ya kiungo ya ukabaji ya Simba ambayo Robertinho amesema anatengeneza mfumo sahihi wa kuweza kuithibiti Al Ahly, kawaida imekuwa ikiongozwa na Fabrice Ngoma, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute huku kiungo cha ushambuliaji mara nyingi kikiwa chini ya Clatous Chama, Kibu Denis na Saido Ntibazonkiza.

Kuhusu maendeleo ya golikipa Aishi Manula ambaye Jumamosi iliyopita Robertinho alimpa dakika 40 wakati wakishinda mabao 5-1 kwenye mechi ya kirafiki ya kimazoezi dhidi ya Dar City FC iliyopigwa Uwanja wa Mo Arena, alisema pamoja na kutaka kuwapa utimamu wa mwili wachezaji wake wote na kuangalia mapungufu, lakini ilikuwa ni kumwangalia kipa huyo kama atakuwa yupo tayari kukaa langoni.

Kipa huyo ambaye aliumia Aprili 7 mwaka huu katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Simba ikishinda mabao 5-1, katika mchezo huo dhidi ya Dar City alionekana kuwa fiti.

Robertinho alisema Manula alionesha kuwa fiti kwa dakika 40 alizocheza kabla ya kumpisha kipa mwingine aliyesajiliwa kutoka KMC, Hussein Abel.

"Amekaa langoni lengo ilikuwa ni kumwangalia kama atakuwa yuko fiti, nimemwona na anaweza kukaa langoni Ijumaa, lakini hiyo pia itategemea pia ushauri wa pamoja

INAENDELEA UKURASA 23



Ngoma

# Gamondi hataki kupoteza mechi tena

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema baada ya kutazama ubora na udhaifu wa Azam FC, amebadilisha programu ya mazoezi kwa wachezaji wake na kutengeneza mifumo ya uchezaji ili kuweza kukabiliana nayo Oktoba 22, mwaka huu katika Uwanja wa Azam Coplex, Chamazi.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema licha ya kutokamilika kwa wachezaji wote ameanza mazoezi ya nguvu na nyota waliopo kuhakikisha wanakuwa imara kwa ajili ya mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, akikiri utakuwa mchezo mkali lakini hatokubali kupoteza kirahisi.

"Kila mchezaji anatambua wajibu wake, tupo vizuri kila nafasi na tunaendelea kuwa imara katika sehemu chache ikiwamo ulinzi na ushambuliaji ambazo zilikuwa na kasoro.

"Kikubwa tunataka ushindi wa mabao mengi mbele ya Azam FC, naamini hata wapinzani wanafanya maandalizi, kwetu tunahitaji kuingia kwa mbinu tofauti na michezo iliyopita kwa sababu tunahitaji kutetea taji," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa hawatoruhusu kupoteza mchezo wa pili kwani kipindi ligi ikiwa mbichi ndio wakati wa kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi zilizopo mbele yao bila ya kujali wanacheza ugenini au nyumbani.

Gamondi alisema kila mechi inakuwa na maandalizi yake na kuelekea mchezo huo wanajiandaa kulingana na ubora wa Azam FC ambao wamekuwa nao kwa sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >